MITAGUSO MIKUU

UTANGULIZI

Yesu Kristo aliwakabidhi mitume kumi na wawili uongozi wa Kanisa wakiwa kundi moja lenye mkuu wake, yaani Petro. Vilevile waandamizi wao, yaani maaskofu wote, ni kundi moja na Papa wa Roma ndiye mkuu wao. Huyo peke yake, na kundi la maaskofu likiwa pamoja naye na chini yake, ndio wenye mamlaka ya juu katika Kanisa lote. Mamlaka hiyo inatumika kwa namna ya pekee unapofanyika mtaguso mkuu, yaani mkutano maalumu wa maaskofu uliokubaliwa na Papa kuwa unawakilisha kundi hilo lote. Hakuna uamuzi wa kudumu kuhusu ipi ni mikuu kati ya mitaguso yote iliyofanyika katika historia ya Kanisa. Tangu karne XVI Wakatoliki wataalamu wa sheria za Kanisa wanatoa orodha yao, ambayo kwa sasa ni kama ifuatavyo.

ORODHA YA MITAGUSO MIKUU

- Katika milenia ya kwanza ilifanyika mashariki (Uturuki wa leo):

1. Nisea I (mwaka 325)
2. Kostantinopoli I (381)
3. Efeso (431)
4. Kalsedonia (451)
5. Kostantinopoli II (553)
6. Kostantinopoli III (680-681)
7. Nisea II (787)
8. Kostantinopoli IV (869-870)

- Katika milenia ya pili ilifanyika magharibi (Italia, Ufaransa, Ujerumani na Uswisi wa leo):

9. Laterano I (1123)
10. Laterano II (1139)
11. Laterano III (1179)
12. Laterano IV (1215)
13. Lyon I (1245)
14. Lyon II (1274)
15. Vienne (1311-1312)
16. Konstanz (1414-1418)
17. Firenze (1431-1445)
18. Laterano V (1512-1517)
19. Trento (1545-1563)
20. Vatikano I (1869-1870)
21. Vatikano II (1962-1965)

HISTORIA YA MITAGUSO MIKUU

Mitaguso mikuu ya kwanza ilifanyika hasa ili kubainisha katika mafundisho yaliyogongana yapi yanalingana na imani sahihi. Mwisho wake ulikuwa kutangaza dogma fulani na kutenga na Kanisa watakaokataa kuiamini na watakaofundisha tofauti.

Mitaguso iliyofanyika baada ya farakano la mwaka 1054 kati ya Kanisa la mashariki na la magharibi, pamoja na kulenga umoja uliovunjika na kufundisha dogma mpya, ilishughulikia zaidi urekebisho wa Kanisa katika ngazi na nyanja zote. Kwa namna ya pekee mtaguso wa pili wa Vatikano tangu uitishwe ulijulikana kuwa wa kichungaji, yaani usio na lengo la kufundisha dogma mpya wala kulaani mafundisho mengine.

Mtaguso wa kwanza wa Nisea (325)

Mtaguso wa kwanza wa Nisea ndio mtaguso wa kwanza kuitwa (tangu mwaka 338) mtaguso wa kiekumeni, yaani mtaguso wa dunia yote au mtaguso mkuu. Ndiyo sababu inashika nafasi ya pekee kati ya mitaguso yote.

Uliitishwa na kusimamiwa na kaisari Konstantino Mkuu, aliyehofia mabishano kati ya raia wake Wakristo kuhusu Yesu Kristo, ambayo yalihatarisha umoja na usalama wa Dola la Roma lililoanza kuelekea kusambaratika. Yeye aliwaalika maaskofu wote wa dola, waliokuwa kama 1000 mashariki na kama 800 magharibi. Washiriki walitokea hata nje ya dola hilo, kama vile Persia na Armenia.

Katika hali hiyo mtaguso ulianza tarehe 20 Mei 325; washiriki walikuwa kama 318, wengi wao wakitokea upande wa mashariki wa dola hilo. Upande wa magharibi uliwakilishwa na watu 4 kutoka Ulaya na 1 kutoka Afrika. Papa Silvesta I (314-335) aliwakilishwa na mapadri wawili.

Asili ya mabishano ilitokea katika Kanisa la Aleksandria (Misri), ambapo kasisi Arios alikuwa amekanusha umungu wa Yesu, na hivyo alihukumiwa na Sinodi ya Aleksandria ya mwaka 321, iliyoitishwa na askofu Aleksanda wa Aleksandria. Hata hivyo Arios hakuacha mafundisho yake, akakimbilia Palestina kwa rafiki yake Eusebio wa Nikomedia.

Basi, mtaguso ulikiri karibu kwa kauli moja kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu kwa maana ana *ousìa* (yaani *dhati*) ileile ya Kimungu aliyonayo Baba. Ndiyo kiini cha Kanuni ya imani ya Nisea iliyopitishwa na mtaguso.

Uamuzi mwingine wa mtaguso ulikuwa kupanga siku ya Pasaka, sherehe kuu ya Kanisa, iwe Jumapili inayofuata mbalamwezi ya kwanza ya majira ya Springi, tofauti na kalenda ya Kiyahudi. Pia zilitungwa kanuni 20 kuratibu mambo mbalimbali.

Mtaguso ulipomalizika tarehe 25 Julai 325, Konstantino alifikiri uamuzi juu ya dogma utamaliza mabishano, lakini haikuwa hivyo, kwa sababu Wagiriki wengi, ingawa hawakukubaliana na Arios, hawakuridhika na msamiati uliotumika kuelezea uhusiano wa Baba na Mwana.

Mtaguso wa kwanza wa Konstantinopoli (381)

Mtaguso wa kwanza wa Konstantinopoli ndio wa pili katika orodha ya mitaguso ya kiekumene wakati wa mababu wa Kanisa. Uliitishwa na kaisari Theodosius I ukafanyika Konstantinopoli mwaka 381.

Maaskofu 150 waliohudhuria walilaani aina mbalimbali za uzushi, hasa ule wa Masedoni wa Konstantinopoli aliyekanusha umungu wa Roho Mtakatifu, wakathibitisha maamuzi ya mtaguso mkuu wa kwanza (Mtaguso wa kwanza wa Nisea), uliofanyika mwaka 325.

Hivyo walikiri kwamba Roho Mtakatifu pia, kama vile Yesu Mwana wa Mungu, anachanga dhati ileile ya Baba.

Pamoja na hayo, walikamilisha kanuni ya imani ya Nisea ambayo kwa sababu hiyo inaitwa sasa kanuni ya imani ya Nisea-Konstantinopoli na ambayo inatumika sana hata leo katika madhehebu mbalimbali ya Ukristo, hasa katika liturujia.

Mtaguso wa Efeso (431)

Mtaguso wa Efeso unahesabiwa na Wakristo walio wengi kama mtaguso mkuu wa tatu. Ulifanyika Efeso katika mkoa wa Asia Ndogo, kwa amri ya kaisari Theodosi II; Papa Selestini I (422-432) alimteua Sirili wa Aleksandria kuuendesha; washiriki walikuwa zaidi ya 150 na kujadili vikali hasa uzushi wa Nestori wa Konstantinopoli.

Patriarki huyo alikuwa anasisitiza ubinadamu wa Yesu Kristo kuliko umungu wake, akisema Bikira Maria alimzaa mtu Yesu, si Mungu, wala si Neno wa Mungu aliyehifadhiwa ndani ya nafsi ya Kristo kama hekaluni. Kwa hiyo Kristo alikuwa *Theophoros*, yaani "mbeba Mungu", na Maria *Christotokos*, "Mama wa Kristo" si *Theotokos*, "Mama wa Mungu".

Mtaguso huo ulilaani haraka mafundisho hayo ukikiri kwamba nafsi ya Yesu Kristo ni moja tu, ile ya milele ya Mwana wa Mungu, na kwamba nafsi hiyo ilitwaa ubinadamu kamili wenye mwili na roho. Hivyo Maria ni *Theotokos* kwa kuwa alimzaa Mungu kama binadamu.

Wajumbe wa Papa walipofika walithibitisha uamuzi huo, lakini maaskofu kutoka Antiokia hawakuridhika, na uzushi huo uliendelea Mesopotamia na kuenea hata Asia mashariki.

Mtaguso ulitangaza kuwa Kanuni ya Imani ya Nisea-Konstantinopoli ni kamili ukakataza isibadilishwe kwa namna yoyote. Pia ulilaani Upelaji, uzushi kutoka Ulaya magharibi kuhusu uwezo wa binadamu kutenda mema bila ya kusaidiwa na neema ya Mungu.

Mtaguso wa Kalsedonia (451)

Mtaguso wa Kalsedonia (leo katika nchi ya Uturuki) unahesabiwa na Wakristo wengi kuwa wa nne kati ya mitaguso ya kiekumeni iliyofanyika katika historia ya Kanisa.

Mtaguso huo uliitishwa na kaisari Marcianus wa Dola la Roma Mashariki pamoja na mke wake Pulkeria wa Bizanti miaka 20 baada ya Mtaguso wa Efeso.

Hao waliona haja ya kudumisha umoja wa Wakristo, uliokuwa msingi wa uimara wa dola hilo, hasa wakati huo ambapo makabila yasiyo na ustaarabu kutoka Asia yalikuwa yanajaribu kuteka Ulaya.

Umoja huo uliingia hatari ya kuvunjika kutokana na uamuzi wa mtaguso mkuu wa Efeso kuhusu imani sahihi juu ya Yesu Kristo kutoeleweka kwa namna moja.

Hasa baadhi ya walioshinda mtaguso huo walionekana kusisitiza mno umungu wake hata kutia shaka kama wanaamini sawasawa ubinadamu wake.

Vikao vilianza tarehe 8 Oktoba 451 vikiwa na washiriki zaidi ya 350: mara nyingi inatajwa idadi ya 600 hivi. Hatimaye mafundisho ya Eutike na Dioskoro wa Aleksandria yalilaaniwa.

Ufanisi wa mtaguso ulichangiwa na msimamo wa kaisari Valentiniano III wa Dola la Roma Magharibi, binamu wa Pulkeria. Kaisari huyo alimuunga mkono Papa Leo I (440-461) aliyekuwa

ametoa msimamo wake na wa Kanisa la Roma tangu mwaka 449 katika *Tomus ad Flavianum,* yaani Waraka kwa Flaviano, Patriarki wa Konstantinopoli aliyeuawa na wafuasi wa Eutike.

Ingawa msimamo huo wa kati ulikubaliwa na wengi, wengine waliuona ni kinyume cha uamuzi wa Efeso, hivyo walishikilia sana mtazamo hao hata walipodhulumiwa na serikali. Ndiyo asili ya farakano la Misri, Syria, Armenia n.k. linalodumu hata leo.

Mtaguso huo ulitunga pia kanuni mbalimbali, kama vile kwa kumpatia Patriarki wa Konstantinopoli nafasi ya pili kati ya maaskofu wote.

Mtaguso wa pili wa Konstantinopoli (553)

Mtaguso wa pili wa Konstantinopoli uliitishwa na kaisari Justiniani I mwaka 553 kwa lengo la kupatanisha tena na Kanisa Katoliki Wakristo wote wa Misri, Syria n.k. waliojitenga miaka 100 iliyopita kufuatana na Mtaguso wa Kalsedonia.

Kwa ajili hiyo kaisari huyo alifanya yalaaniwe maandishi ya Wanestori watatu (Teodoro wa Mopsuestia, Teodoreto wa Kiro na Iba wa Edesa) yaliyochukiwa sana na Wamisri.

Pia mtaguso mkuu huo ulilaani baadhi ya mafundisho wa Origene.

Walihudhuria maaskofu 168; kati yao 11 walitokea magharibi. Kumbe Papa Vigili (537-555) na maaskofu wengine 12 wa magharibi walikataa kuhudhuria ingawa walikuwepo Konstantinopoli, ila mwaka uliofuata alikubali maamuzi ya mtaguso.

Hatimaye Papa Gregori I (590-604) aliutambua kama mtaguso mkuu kwa sababu haukuharibu kitu. Hivyo Wakristo wengi wanahesabu mtaguso huo kuwa wa tano kati ya Mitaguso ya kiekumeni, ingawa lengo halikufikiwa, kwa kuwa Wamisri waliendelea kukataa mtaguso wa Kalsedonia.

Mtaguso wa tatu wa Konstantinopoli (680-681)

Mtaguso wa tatu wa Konstantinopoli unahesabiwa na Wakristo wengi kuwa wa sita kati ya Mitaguso ya kiekumeni.

Kaisari Konstantino IV wa Konstantinopoli ndiye aliyeuitisha na kuuendesha kuanzia tarehe 7 Novemba 680 hadi tarehe 16 Septemba 681.

.Suala kuu lililosumbua Wakristo wa karne VII lilimhusu Yesu Kristo upande wa utashi. Ulikuwa unaenea mtazamo wa kwamba hakuwa na utashi wa kibinadamu, bali ule wa Kimungu tu.

Lakini wamonaki Sofronio wa Yerusalemu na Maksimo Muungamadini walipinga vikali jaribio hilo la kuleta upatanisho wa Waorthodoksi wa Mashariki (Wamisri n.k.) kwa kumpunguza Yesu katika ubinadamu wake kamili uliosisitizwa na Mtaguso wa Kalsedonia (451).

Vilevile Papa Martin I (649-655), katika mtaguso uliofanyika Laterani, alilaani mtazamo huo, kinyume cha Kaisari na Patriarki wa Konstantinopoli.

Konstantino IV alikubaliana na Papa Agatoni (678-681), na hivyo Mtaguso wa tatu wa Konstantinopoli ulilaani rasmi mtazamo wa kwamba Yesu hakuwa na utashi wa kibinadamu.

Mtaguso wa pili wa Nisea (787)

Mtaguso wa pili wa Nisea uliitishwa na malkia Irene wa Bizanti mwaka 787 ili kujadili matumizi ya sanamu katika Ukristo, kutokana na ombi la Papa Adrian I (772-795).

Wakristo wengi wanauhesabu kuwa wa saba kati ya Mitaguso ya kiekumeni. Ni wa mwisho kufanyika wakati wa mababu wa Kanisa.

Mtaguso mkuu huo ulihitajika ili kumaliza mabishano makali kuhusu sanamu za Kikristo yaliyochukua zaidi ya miaka 100 hasa katika Dola la Roma Mashariki yakimalizika mwaka 843 tu.

Chanzo ni uamuzi wa kaisari Leo III wa Konstantinopoli (717-741) wa kuteketeza sanamu zote ili kujilinganisha na Waislamu waliotishia utawala wake.

Patriarki wa Konstantinopoli alilazimika kujiuzulu, lakini uamuzi wa kaisari ulizidi kupingwa hasa na wamonaki na mwanateolojia Yohane wa Damasko. Mapapa wa Roma pia walipinga uamuzi huo.

Sera ya dola ilibadilika aliposhika uongozi Irene kwa niaba ya mtoto wake mdogo Konstantino VI.

Mtaguso ulianza Konstantinopoli mwaka 786, lakini ulipoingiliwa na jeshi waliowaunga mkono maaskofu wengi waliopinga sanamu, Irene aliuhamishia Nisea ambapo vilifanyika vikao 7 kuanzia tarehe 28 Septemba 787. Cha mwisho kilifanyika katika ikulu tarehe 23 Oktoba 787.

Pamoja na maaskofu 300 hivi wa dola hilo, walihudhuria wamonaki wengi. Papa alituma mabalozi wake wawili na barua moja.

Mtaguso ulitofautisha heshima inayokubalika kwa sanamu na ibada isiyovumilika. Hoja kuu ni kwamba sanamu si kitu, ila inamwakilisha yule aliyechorwa ndani yake. Kimsingi sanamu zinakubalika kutokana na umwilisho wa Mwana wa Mungu uliomfanya atwae sura na kuonekana.

Mtaguso ulichukua pia maamuzi mbalimbali ili kurekebisha Kanisa.

Mtaguso wa nne wa Konstantinopoli (869-870)

Mtaguso wa nne wa Konstantinopoli ni jina linalotumiwa na Wakristo kwa namna tofauti, kadiri wanavyokubali au kukataa uhalali na uekumeni wa mitaguso fulanifulani.

Kanisa Katoliki linahesabu kuwa Mtaguso mkuu wa nne wa Konstantinopoli ule uliofanyika tangu tarehe 5 Oktoba 869 hadi 28 Februari 870.

Uliitishwa na Kaisari Basili I wa Konstantinopoli na Papa Adrian II (867-872), kwa sababu mwisho wa ikonoklastia katika sinodi ya mwaka 843 ulikuwa umeacha athari kubwa katika Kanisa la Mashariki.

Patriarki Metodi wa Konstantinopoli (843-847) alijitahidi kutuliza pande zote, lakini hakufaulu.

Alipofariki, malkia Teodora, akitawala kwa niaba ya mtoto Mikaeli III, alilazimisha nafasi yake ishikwe na Ignas I, mmonaki mwenye msimamo mkali, ambaye hatimaye aliondoshwa.

Badala yake alichaguliwa mlei msomi Fosyo ambaye kwa siku chache alipewa daraja na kutawazwa, lakini kufikia Februari 859 lililotea farakano kati ya waliomkubali yeye na waliomkubali Ignas I.

Ndipo Fosyo alipojitahidi kuungwa mkono na Papa Nikolaus I (858-867), ambaye kwanza alimkubali pamoja na pendekezo la Kaisari Mikaeli III la kuitisha mtaguso uliofanyika Konstantinopoli kati ya Aprili na Agosti 861 wakihudhuria maaskofu zaidi ya 300.

Papa hakupendezwa na maamuzi ya mtaguso huo, akashindana na Kaisari kimaandishi kwa sababu za kiutamaduni na za kisiasa pia.

Hapo Fosyo alipata nguvu dhidi ya Papa akaitisha mtaguso uliovunja umoja kati ya Makanisa ya Mashariki na yale ya Magharibi mwaka 867, akithubutu kwa mara ya kwanza kumhukumu Papa kama mzushi na kutaka kumuondoa madarakani.

Kumbe Kaisari mpya alimrudisha Ignas I kuwa Patriarki na pamoja naye akamuomba Papa atume mabalozi kwa mtaguso mwingine wa kufanyika Konstantinopoli.

Mtaguso ulipoanza tarehe 5 Oktoba 869 walikuwepo tu maaskofu wakuu 5 na maaskofu wengine 7, lakini walikuwepo mabalozi wa Mapatriarki wa Antiokia na Yerusalemu (wale wa Aleksandria walifika baadaye).

Waliokuwa upande wa Fosyo walikubaliwa kuhudhuria kuanzia tarehe 7 Oktoba wakamtetea sana dhidi ya msimamo wa Papa, lakini wakashindwa na kutengwa (29 Oktoba).

Baada ya miezi mitatu mtaguso uliendelea tarehe 12 Februari 870, wakiwepo maaskofu 67 walioongezeka tena hadi kufikia 103 siku ya mwisho (28 Februari), lilipotolewa tamko la imani pamoja na kanuni 26 kuhusu teolojia na sheria, bila ya kutoa mafundisho mapya. Pamoja na idadi yenyewe kutokuwa kubwa sana, ni muhimu kwamba walikuwepo maaskofu wakuu 37 kati ya 40.

Kwa kuwa mtaguso huu haukukubaliwa sana huko Konstantinopoli (hasa baada ya Fosyo kurudia Upatriarki mwaka 877), na pande mbili zilishindwa zaidi na zaidi kuelewana, uliitishwa mtaguso mwingine, ambapo wafuasi wa Fosyo walikuwa ndio wengi.

Baadhi ya Waorthodoksi wanahesabu mtaguso huo mpya (879-880), uliofuta maamuzi dhidi ya Fosyo, kuwa wa kiekumeni na kuukataa ule wa miaka 10 ya nyuma. Lakini wengine hawakubali kuwa wa kiekumeni kwa sababu haukutoa mafundisho ya imani.

Ingawa wajumbe wa Papa Yohane VIII (872-882) walikubali kwanza maamuzi wa mtaguso huo ili kudumisha amani, na labda hata yeye mwenyewe, waandamizi wake waliukataa, na Fosyo mwenyewe aliondoshwa tena mwaka 886.

Mtaguso wa kwanza wa Laterano (1123)

Mtaguso wa kwanza wa Laterano unahesabiwa na Kanisa Katoliki mtaguso mkuu wa tisa katika historia yake, wa kwanza kufanyika Magharibi. Ulianza tarehe 18 Machi ukamalizika tarehe 11 Aprili 1123.

Mahali pake ni kwenye Kanisa kuu la Roma huko Laterano, mtaa wa Roma (Italia) alipokuwa anaishi askofu wake. Hukohuko baadaye ilifanyika mitaguso mingine minne ya Karne za Kati. Umuhimu wake ulipungua hasa baada ya Papa kuhamia Vatikano.

Mtaguso uliitishwa na Papa Kalisti II (1119-1124) mnamo Desemba 1122, mara baada ya Mapatano ya Worms, ya kwanza kufanyika kati ya Papa na Dola Takatifu la Kirumi, iliyofurahisha sana wanakanisa, hata mwaka huo ulitajwa kuwa mwanzo wa kipindi kipya.

Mapatano hayo yalikomesha desturi ya walei kuteua viongozi wa Kanisa na wa utawa, yakitenganisha shughuli za kiserikali na zile za kidini, na kukubali kwamba mamlaka ya kiroho inatokana na daraja takatifu.

Ili kuthibitisha mapatano hayo, Papa alialika Roma maaskofu wote wa Magharibi. Waliohudhuria kweli walikuwa zaidi ya 900 kati ya maaskofu zaidi ya 300 na maabati 600 hivi). Papa mwenyewe aliendesha vikao.

Hakuna hati za mtaguso, ila matunda yake. Tunachojua ni kwamba Mapatano hayo yalisomwa yakapitishwa rasmi, pamoja na kanuni 22 au 25, ambazo nyingi zilikuwa zimeshapitishwa zamani.

Mtaguso wa pili wa Laterano (1139)

Mtaguso wa pili wa Laterano, uliofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 11 Aprili 1139 chini ya Papa Inosenti II (1130-1143), unahesabiwa na Kanisa Katoliki kuwa mtaguso mkuu wa kumi. Ni wa pili kufanyika Magharibi, kwenye Kanisa kuu la Roma (Italia).

Mtaguso ulihitajika kutokana na farakano lililotokea mwaka 1130 alipofariki Papa Honori II (1124-1130): hapo makardinali waligawanyika kuhusu Mapatano ya Worms, ambayo mwaka 1122 yalikuwa yamekomesha mashindano kuhusu uteuzi wa maaskofu.

Isitoshe, kulikuwa na ushindani kati ya koo mbili za Roma, yaani Frangipane na Pierleoni.

Tarehe 14 Februari 1130, makardinali 16 waliosimama upande wa familia ya Frangipane walimchagua Gregorio Papareschi, aliyejiita Papa Inosenti II.

Saa chache baadaye, Pietro Pierleoni alichaguliwa na makardinali wengine na kujiita papa Anakleti II.

Hatimaye, kwa msaada wa Bernardo wa Clairvaux, Inosenti II alishinda na kukubaliwa na wengi, ingawa hakuweza kuhamia Roma mpaka baada ya mpinzani wake kufa (1138).

Mtaguso ulipaswa kurekebisha matokeo ya farakano hilo. Basi, Inosenti II alifungua kikao na kuondoa madarakani maaskofu waliomfuata mpinzani wake.

Halafu papa alikusudia kuendeleza juhudi za urekebisho za Mtaguso wa kwanza wa Laterano. Hivyo zikapitishwa kanuni 30, ambazo nyingi kati yake zilikuwa za kurudia zile za zamani kuhusu usimoni, mapadri wenye wake n.k.

Mtaguso wa tatu wa Laterano (1179)

Mtaguso wa tatu wa Laterano uliitishwa na Papa Aleksanda III (1159-1181) ufanyike huko Roma mwaka 1179, kutokana na Amani ya Venezia kati ya Kaisari Federiko I wa Ujerumani na Lega Lombarda ya Italia kaskazini.

Unahesabiwa na Kanisa Katoliki kama mtaguso mkuu wa kumi na moja. Ulijadili masuala mbalimbali na kuyatungia kanuni. Kati ya maamuzi muhimu zaidi, mmojawapo ulihusu uchaguzi wa Papa, ukidai thuluthi mbili za kura za makardinali wote, bila ya kutofautisha haki za makundi yao matatu.

Mtaguso wa nne wa Laterano (1215)

Mtaguso wa nne wa Laterano unahesabiwa na Kanisa Katoliki kama mtaguso mkuu wa 12.

Uliitishwa na Papa Inosenti III (1198-1216) kama kilele cha kazi yake.

Ulihudhuriwa na maaskofu zaidi ya 400 (wakiwemo mapatriarki wa Kilatini wa Konstantinopoli na Yerusalemu na wawakilishi wa wale wa Antiokia na Aleksandria), na wakuu wa watawa zaidi ya 800, mbali na mabalozi wa watawala wa nchi mbalimbali.

Mada kuu zilikuwa Vita vya msalaba, Mashindano kuhusu uteuzi wa viongozi wa Kanisa, mamlaka ya Papa, mwenendo wa makleri, mashirika ya kitawa, imani (kuhusu ekaristi n.k.) na wajibu wa Wakristo wote kupokea sakramenti ya kitubio walau mara moja kwa mwaka.

Kutokana na wingi na umuhimu wa mafundisho na maamuzi yaliyotolewa, mtaguso huo unahesabiwa kuwa kati ya ile iliyoathiri zaidi Kanisa hadi leo.

Mtaguso wa kwanza wa Lyon (1245)

Mtaguso wa kwanza wa Lyon uliitishwa na Papa Inosenti IV (1243-1254) tarehe 24 Juni 1245 akiwa huko Lyon (Ufaransa), alipokimbilia usalama. Waliushiriki karibu viongozi 150 wa Kanisa Katoliki, ambalo linauhesabu kuwa mtaguso mkuu wa 13.

Baada ya mashindano makali kati ya mamlaka ya kiroho ya Papa na ile ya kisiasa ya kaisari huko Ulaya, mtaguso huo uliitishwa ili kumhukumu moja kwa moja kaisari Federiko II kuwa Mpinga Kristo.

Mtaguso ulianza tarehe 28 Juni 1245 wakiwepo maaskofu 144, halafu ukawa na vikao viwili vingine tena tarehe 5 Julai na 17 Julai. Hatimaye maaskofu walikuwa 225.

Mwanzoni papa alitangaza matatizo 5 yanayotesa Kanisa:

- kuharibika kwa imani na maadili;
- kushindwa kuikomboa Nchi takatifu (Yerusalemu ulitekwa tena na Waturuki mwaka 1244);
- kudumu kwa farakano la Waorthodoksi;
- kujitokeza hatari ya kuvamiwa na Watartari;
- kupambana na Federiko II.

Maamuzi yalitangazwa tarehe 25 Agosti tu, baada ya papa na wasaidizi wake kurekebisha miswada, yakapokewa na kufafanuliwa na vyuo vikuu. Lakini uamuzi wa kumuondoa madarakani kaisari haukuweza kutekelezwa hata kwa vita.

Mtaguso wa pili wa Lyon (1274)

Mtaguso wa pili wa Lyon, uliofanyika mwaka 1274, unahesabiwa na Kanisa Katoliki kama mtaguso mkuu wa 14.

Mtaguso wa pili kufanyika Lyon (Ufaransa) ulikusudiwa hasa kurudisha umoja kamili kati ya Wakatoliki na Waorthodoksi, uliotafutwa katika karne ya 13 yote.

Mnamo Februari 1274, katika ikulu ya Konstantinopoli, kaisari Mikaeli VIII ilifaulu kufanya maaskofu wengi wakiri ungamo la imani lililodaiwa na Papa Klementi IV (1265-1268).

Ndipo Papa Gregori X (1271-1276) alipoitisha mtaguso huko Lyon, ambao uhudhuriwe na wawakilishi wa Waorthodoksi ili kukamilisha umoja.

Papa Gregori X alifungua mtaguso tarehe 7 Mei 1274 akitangaza tena malengo yake matatu:

- kusaidia Wakristo wa Nchi takatifu,
- kuungana tena na Waorthodoksi,

- kurekebisha maadili ndani ya Kanisa.

Vilifuata vikao viwili tarehe 18 Mei na 4 Juni. Halafu tarehe 24 Juni ulifika na kupokewa kwa shangwe ujumbe kutoka Ugiriki, ukiundwa na maaskofu 2 na katibu wa kaisari.

Tarehe 6 Julai kilifanyika kikao cha nne kwa ajili ya muungano na hatimaye tarehe 16 Julai kile cha mwisho kilichopitisha hati mbalimbali za urekebisho. Kesho yake mtaguso ulifungwa.

Muungano haukuweza kudumu, kwa sababu, alivyoandika Papa Paulo VI (1963-1978) tarehe 19 Oktoba 1974, ulifanyika «bila ya kulipatia Kanisa la Kigiriki nafasi ya kutokeza kwa hiari mtazamo wake kuhusu jambo hilo. Wakristo wa Kilatini ndio waliotunga hati na matamko kufuatana na mafundisho juu ya Kanisa yaliyofafanuliwa na kupangwa magharibi».

Mikaeli VIII alijaribu kulazimisha raia zake wapokee mambo wasiyoyakubali kwa moyo, hata akatumia nguvu kuwadhulumu waliokataa; akilaumiwa na watu wa Roma kwa kushindwa kufanikisha muungano, akaja kutengwa na Kanisa. Alipokufa (1282), mwanae Andronikо II aliyemrithi, alifuta maamuzi ya baba yake kwa ajili ya muungano.

Vilevile mipango kwa ajili ya vita vya msalaba haikutekelezwa, na hatimaye (1291) Waturuki waliteka Akri, mji wa mwisho kubaki mikononi mwa Wakristo huko Mashariki ya Kati.

Maamuzi mengine yalihusu utaratibu mpya wa kumchagua Papa kwa lengo la kuzuia uchelewaji uliojitokeza hapo nyuma, na katazo la mashirika mapya ya kitawa.

Mtaguso wa Vienne (1311-1312)

Mtaguso wa Vienne unahesabiwa na Kanisa Katoliki kama mtaguso mkuu wa 15.

Mtaguso huu ulifanyika Vienne (Ufaransa) baada ya mashindano kati ya Papa Bonifas VIII (1294-1303) na mfalme wa Ufaransa Filipo IV.

Hatimaye mwaka 1309 mwandamizi wake, Papa Klementi V (1305-1314) alikubali kubaki Avignon (leo nchini Ufaransa), karibu na himaya ya mfalme huyo.

Mapapa walibaki huko hadi mwaka 1377, waliporudi Roma.

Kwa shinikizo la mfalme, Papa alitoa hati *Regnans in excelsis* (12 Agosti 1308) ili kuitisha mtaguso mkuu huko Vienne tarehe 1 Novemba 1310, kwa lengo la kujadili mada 4:

- suala la Wahekalu;
- vita vya msalaba;
- hali ya imani na Kanisa kwa jumla;
- urekebisho wa Kanisa.

Mtaguso ulichelewa kuanza hadi tarehe 16 Oktoba 1311, walipokuwepo washiriki 170 hivi, ambao kati yao Wafaransa walikuwa zaidi ya thuluthi moja. Wengine walizuiwa na mfalme wa Ufaransa.

Vikao rasmi vikawa vitatu hadi Machi 1312.

Kuhusu Wahekalu, Mtaguso uliamua kufuta shirika lao kama alivyopenda mfalme, bila ya kulifanyia utafiti wala kulitolea hukumu.

Kuhusu Vita vya msalaba, Mtaguso uliamua kuvianza upya na kwa ajili hiyo kutoza zaka kwa miaka sita, lakini mfalme alijitwalia hizo pesa bila ya kutekeleza ahadi yake ya kuongoza vita hivyo.

Kuhusu imani, Mtaguso ulijadili baadhi ya mafundisho hasa ya makundi kadhaa ya watawa, lakini uamuzi ulichukuliwa baadaye tu.

Kuhusu urekebisho, Mtaguso ulidai haki za Kanisa ziheshimiwe na serikali za nchi. Pia ulijadili kirefu mahusiano ya ndani, hasa kati ya maaskofu, maparoko na watawa.

Mtaguso wa Konstanz (1414-1418)

Mtaguso wa Konstanz (Ujerumani) unahesabiwa na Kanisa Katoliki kama mtaguso mkuu wa 16.

Mtaguso huu uliitishwa na antipapa Yohane XXIII kwa ombi la kaisari Sigismund wa Ujerumani ukathibitishwa na Papa Gregori XII (1406-1415).

Lengo kuu lilikuwa kumaliza Farakano la Magharibi lililofikia hatua ya kuona maaskofu watatu kujidai Papa kwa wakati mmoja. Malengo mengine yalikuwa kung'oa uzushi na kurekebisha Kanisa "katika kichwa na viungo vyake".

Hatimaye Papa Gregori XII alikubali kujiuzulu, wapinzani wake wawili waliondolewa, na Papa Martin V akachaguliwa.

Ulikuwa mtaguso muhimu kwa wingi wa waliohudhuria (makardinali 29, maaskofu 186, maabati zaidi ya 100 na wataalamu 300 hivi), muda (vikao 55) na mafanikio, ingawa majaribio yake ya mapinduzi yalishindikana, hasa ulipodai kuwa na mamlaka ya juu kuliko Papa.

Kati ya maamuzi mengine kuna hukumu dhidi ya John Wyclif and Jan Hus kama wazushi.

Mtaguso wa Firenze (1431-1445)

Mtaguso wa Firenze uliitishwa na Papa Martin V (1417-1431) mwaka wa mwisho wa uongozi wake) ili kutekeleza shingo upande agizo la Mtaguso wa Konstanz la kwamba mtaguso ufanyike mara kwa mara.

Mtaguso ulianza Basel (Uswisi) chini ya Papa Eugenio IV (1431-1447), ukiwa na maaskofu wachache kulingana na mapadri na walei wenye haki ya kupiga kura.

Ingawa mtaguso ulifaulu kupatanisha wafuasi wa Hus na Kanisa, na kutoa sheria kadhaa za urekebisho kwa kibali cha Papa, baadaye ulianza kumshambulia yeye pamoja na makardinali, ukionyesha wazi wengi waliuona una mamlaka ya juu kuliko Papa, kinyume cha mapokeo.

Hapo Eugenio IV aliuvunja halafu akauhamishia Ferrara (Italia), ulipokutanika tarehe 8-1-1438, bila ya kujali upinzani wa wale ambao walibaki Basel na kumchagua antipapa wa mwisho, Felix V.

Huko Italia ulifika ujumbe mkubwa kutoka Konstantinopoli kwa ajili ya kurudisha umoja kati ya Kanisa Katoliki na Waorthodoksi. Kati ya wajumbe 700 kulikuwa na kaisari na patriarki wa Konstantinopoli, walioogopa Waturuki watateka mji wao (kama ilivyotokea kweli tarehe 29 Mei 1453); hivyo walihitaji msaada wa Wakristo wenzao wa magharibi.

Ferrara iliachwa kutokana na uhaba wa majengo na hofu ya tauni.

Mwaka 1439 mtaguso ulihamia Firenze ukafikia makubaliano ya kurudisha umoja (6-7-1439), ingawa uamuzi ukashindwa kutekelezwa kwa kiasi kikubwa kutokana na upinzani wa waumini wa Konstantinopoli.

Vilevile tarehe 22-11-1439 yalifikiwa makubaliano na Waarmenia na tarehe 4-2-1440 yale na Wamisri.

Hatimaye tarehe 24-9-1443 mtaguso ulihamia Roma kwenye Laterano. Huko yalifikiwa makubaliano ya kurudisha umoja na Wasiria kadhaa (30-4-1444) na Wakaldayo na Wamaroni wa Kupro (7-8-1445).

Hakuna hati kuhusu mwisho wa mtaguso. Lakini waliobaki Basel na kujitenga na Papa, kufikia tarehe 19-4-1449 walimkubali Nikolaus V na siku sita baadaye walifunga mkutano wao.

Mtaguso huo ulichochea Wakristo wa magharibi kutamani mawasiliano na wenzao wa Ethiopia na India, jambo lililowafanya waanze zile safari za mbali kupitia baharini zilizowafikisha Afrika Kusini na Mashariki, China na Amerika.

Mtaguso wa tano wa Laterano (1512-1517)

Mtaguso wa tano wa Laterano ulifanyika kuanzia mwaka 1512 hadi 1517 huko Roma (Italia), kwenye Basilika la Mt. Yohane huko Laterano ambalo ndilo kanisa kuu la Jimbo Katoliki la Roma.

Kanisa Katoliki linauhesabu kama mtaguso mkuu wa 18.

Uliitishwa na Papa Julius II (1503-1513) ambaye alianza kuusimamia tarehe 3 Mei 1512. Baada ya kifo chake, uliendelezwa na Papa Leo X (1513-1521) hadi kikao cha 12 na cha mwisho kilichofanyika tarehe 16 Machi 1517.

Ulihudhuriwa na maaskofu 100 hivi, wengi wao wakitokea Italia. Kutofika kwa wajumbe kutoka nchi nyingine, pamoja na wengi kukosa nia ya kujirekebisha, kulichangia kufanya utekelezaji wa maamuzi ya mtaguso ushindikane.

Maamuzi hayo yalitolewa kwa hati za Papa. Mengine yanahusu mafundisho ya imani, mengine maagizo ya urekebisho wa Kanisa.

Kabla yake kilifanyika "Kitaguso" cha Pisa: kwa kuwa Papa Julius II alikuwa hatekelezi kiapo chake cha kuitisha mtaguso kwa ajili ya urekebisho, baadhi ya makardinali, wakihimizwa na watawala wa Ujerumani na Ufaransa, waliuitisha huko Pisa (Italia) kuanzia tarehe 1 Septemba 1511. Walikusanyika wachache tarehe 1 Oktoba, halafu katika kikao cha nane walimsimamisha Papa wakahamia Lyon (Ufaransa).

Papa aliitikia “kitaguso” hicho kwa hati ya tarehe 18 Julai 1511, ambayo pamoja na kukipinga na kujitetea aliitisha mtaguso mkuu ukusanyike tarehe 19 Aprili 1512 huko Laterano.

Vita vilichelewesha mwanzo wa mtaguso wenyewe hadi tarehe 3 Mei 1512, walipokusanyika katika basilika la Laterano makardinali 15, mapatriarki 2, maaskofu wakuu 10, maaskofu 56, maabati na wakuu wa mashirika ya kitawa wachache pamoja na mabalozi wa nchi 3. Mwisho walikuwepo makardinali 23 na maaskofu 122.

Upande wa matokeo, utekelezaji wa maagizo ya mtaguso ulikuwa mdogo sana, la sivyo pengine Matengenezo ya Kiprotestanti yasingetokea. Ukweli ni kwamba Martin Luther aliyaanzisha miezi sita tu baada ya mtaguso kwisha.

Mtaguso wa Trento (1545-1563)

Mtaguso wa Trento (uliofanyika kwa kwikwi kuanzia mwaka 1545 hadi 1563), unahesabiwa na Kanisa Katoliki kuwa mtaguso mkuu wa 19.

Mtaguso huo, uliochukua muda mrefu kuliko yote ya historia, ulieneza urekebisho wa Kanisa na kuchukua msimamo kuhusu mafundisho ya Waprotestanti waliojitokeza katika hiyo karne ya 16.

Mtu wa kwanza kulilia mtaguso ambao uamue kati yake na papa alikuwa Martin Luther (1517): huko Ujerumani ombi lake liliungwa mkono na wengi, pamoja na kaisari Karolo V aliyeuona kuwa njia ya kurekebisha Kanisa lakini pia ya kujiimarisha kimamlaka. Ndiyo sababu kuu iliyomfanya Papa Klementi VII (1523-1534), aliyesimama upande wa Ufaransa, kukataa kabisa kuuitisha.

Wazo hilo lilipata nguvu tena chini ya mwandamizi wake, Papa Paulo III (1534-1549), ambaye mwaka 1536 aliitia kwanza Mantova halafu Vicenza maaskofu na maabati wote, pamoja na wafalme wadogo wengi wa Dola takatifu la Kijerumani.

Baada ya juhudi mbalimbali kushindikana, mwaka 1542 uamuzi ulifikiwa wa kuitisha mtaguso huko Trento kwa sababu ni mji wa Italia lakini ulikuwa ndani ya mipaka ya dola hilo. Hatimaye (Novemba 1544) papa aliweza kutoa hati ya kuitisha mtaguso inayoitwa *Laetare Jerusalem*.

Mtaguso ulifunguliwa rasmi tarehe 13 Desemba 1545 katika kanisa kuu la Mt. Vigilio.

Mwanzoni mtaguso ulikuwa na maaskofu wachache, karibu wote kutoka Italia, ukatawaliwa na wajumbe wa papa. Kati ya makardinali wapya (Contarini, Sadoleto, Carafa, Fisher na huyo Pole) wengi walipenda urekebisho.

Zilijadiliwa na kupitishwa hasa dogma dhidi ya mafundisho ya Waprotestanti, kama vile kuhusu utakaso na wokovu. Pamoja na kupitisha tafsiri rasmi ya Biblia katika Kilatini iliyo maarufu kwa jina la Vulgata, kati ya maamuzi muhimu zaidi upo ule wa kudai maaskofu waishi katika majimbo yao ili kufanya uchungaji uliowapasa.

Baada ya mtaguso kuhamishiwa Bologna, Papa Paulo III aliusimamisha mnamo Septemba 1549.

Papa Julius III (1550-1555) aliuitisha tena kuanzia tarehe 1 Mei 1551 na zikatolewa hati juu ya sakramenti za Ekaristi, Kitubio na Mpako wa wagonjwa. Polepole waliohudhuria waliongozeka, wakiwemo Waprotestanti wengi pia, wakidai wanateolojia wao wawe na haki ya kupiga kura na hati zilizokwishatolewa zifutwe. Ndipo ilipoonekana wazi kwamba tofauti katika imani ni kubwa mno.

Majeshi ya Kiprotestanti yalipokaribia Trento, Papa alikubali kusimamisha tena mtaguso tarehe 28 Aprili 1552.

Sehemu ya mwisho ya mtaguso baada ya kuitishwa ilichelewa kuanza hadi tarehe 18 Januari 1562, tena ilikabili matatizo mengi, lakini iliokolewa na kutawaliwa na askofu wa Milano Karolo Borromeo, ndugu wa Papa Pius IV (1559-1565) aliyemalizia haraka mtaguso wakiwemo wajumbe 255.

Katika sehemu hiyo yalitolewa mafundisho rasmi kuhusu Misa, Daraja takatifu na Ndoa, Toharani, sala kwa watakatifu, heshima kwa masalia na rehema. Pia Kanisa la Roma lilikubaliwa kama mama na mwalimu wa makanisa yote. Maaskofu wote walitakiwa kuahidia utiifu kwa Papa, ambaye peke yake ana haki ya kuitisha mtaguso mkuu. Kwa msingi huo, mtaguso ulimuachia Papa kuthibitisha maamuzi yote, naye alifanya hivyo bila ya kujali upinzani wa maofisa wake huko Roma.

Isitoshe, mwishoni, maamuzi mbalimbali yaliachwa mikononi mwa Papa na ofisi zake, yakachukuliwa miaka iliyofuata; kati yake, urekebisho wa Breviari na Misale, kwa kusawazisha liturujia za majimbo ya magharibi (isipokuwa chache, kama ya Milano na Lyon) kulingana na mapokeo ya Roma. Halafu ikatolewa Katekisimu ya Trento na Orodha ya vitabu vilivyokatazwa (Index librorum prohibitorum).

Mtaguso wa kwanza wa Vatikano (1869-1870)

Mtaguso wa kwanza wa Vatikano unatazamwa na Kanisa Katoliki kama Mtaguso Mkuu wa 20 katika historia yake.

Uliitishwa rasmi na Papa Pius IX (1846-1878) mnamo 29 Juni 1867 na vikao vyake viliendelea katika Basilika la Mt. Petro huko Vatikano mjini Roma kuanzia tarehe 8 Desemba 1869 hadi vilipokatika mnamo 1870, kutokana na jeshi la Italia kuteka Roma tarehe 20 Septemba.

Walishiriki maaskofu na mapadri 774 (kati ya 1050 wenye haki ya kuhudhuria), ambao kwa mara ya kwanza walitokea mabara yote. Pia ilikuwa mara ya kwanza ya kutokuwepo wawakilishi wa serikali. Kumbe wajumbe wa Waorthodoksi na wa Waprotestanti walialikwa pia, lakini hawakufika.

Tarehe 24 Aprili 1870, baada ya majadiliano mengi, ilipitishwa hati *Dei Filius* juu ya Mungu, ufunuo, imani, na uhusiano kati ya imani na akili.

Ingawa lengo halikuwa hilo, tokeo kuu la kazi ya mtaguso huo ni tangazo la dogma ya Papa kuwa na karama ya kutokosea katika mafundisho ya imani na maadili anayoyatoa ili yadumu moja kwa moja pale anapotimiza masharti fulani (kwa kifupi: akisema "ex cathedra", yaani "kutoka ukulu).

Dogma hiyo iliimarisha mamlaka ya Papa na umoja wa Kanisa dhidi ya maelekeo ya kitaifa ambayo yalitawala karne zilizotangulia yakisababisha matatizo mengi.

Mtaguso wa pili wa Vatikano (1962-1965)

Malengo ya mtaguso wa pili wa Vatikano

Muda mfupi baada ya kuchaguliwa Papa mwenye heri Yohane XXIII alitangaza uamuzi wake wa kuitisha mtaguso mkuu akiamini kwamba utaweza kuandaa na kusababisha ustawi mpya wa maisha ya Kanisa. Lengo kuu la mtaguso lilikuwa kuliamsha Kanisa likumbuke wito wake na kwa kujifanya upya kwa ndani lipate msukumo mpya wa kimisionari ili kuwatangazia watu wote ujumbe wa milele wa wokovu, amani na umoja.

Tangazo hilo lilitolewa tarehe 25-1-1959. Baada ya maandalizi mtaguso wa pili wa Vatikano ulifunguliwa tarehe 11-10-1962. Vikao vinne vikafanyika mpaka ulipofungwa tarehe 8-12-1965. Kila kikao kilianza Oktoba na kumalizika Desemba ya miaka hiyo.

Kwa kuwa Yohane XXIII alifariki tarehe 2-6-1963, vikao vitatu vya mwisho viliongozwa na mwandamizi wake, Paulo VI, na hati zote kumi na sita zikatolewa chini yake pia kwa kupigiwa kura ya ndiyo karibu kwa kauli moja. Maaskofu na wakuu wa mashirika kadhaa wenye haki ya kupiga kura walikuwa kama elfu tatu, wakiwakilisha karibu Kanisa lote duniani, isipokuwa nchi zile zenye kuwadhulumu Wakristo.

Orodha ya hati 16 za mtaguso

HADHI	JINA LA KILATINI	KIFUPISHO	YAHUSUYO	TAREHE
KATIBA	1. Sacrosanctum Concilium	SC	Liturujia takatifu	4-12-1963
	2. Lumen Gentium	LG	Kanisa	21-11-1964
	3. Dei Verbum	DV	Ufunuo wa Kimungu	18-11-1965
	4. Gaudium et Spes	GS	Kanisa katika ulimwengu wa kisasa	7-12-1965
MAAGIZO	1. Inter Mirifica	IM	Vyombo vya upashanaji habari	4-12-1963
	2. Orientalium Ecclesiarum	OE	Makanisa katoliki ya mashariki	21-11-1964
	3. Unitatis Redintegratio	UR	Ekumeni	21-11-1964
	4. Christus Dominus	CD	Huduma ya kichungaji ya maaskofu	28-10-1965
	5. Perfectae Caritatis	PC	Kurekebisha upya maisha ya kitawa	28-10-1965
	6. Optatam Totius	OT	Malezi ya kipadri	28-10-1965
	7. Apostolicam Actuositatem	AA	Utume wa walei	18-11-1965
	8. Ad Gentes	AG	Utendaji wa kimisheni wa Kanisa	7-12-1965
	9. Presbyterorum Ordinis	PO	Huduma na maisha ya kipadri	7-12-1965
MATAMKO	1. Gravissimum Educationis	GE	Malezi ya Kikristo	28-10-1965
	2. Nostra Aetate	NA	Uhusiano wa Kanisa na dini zisizo za Kikristo	28-10-1965
	3. Dignitatis Humanae	DH	Uhuru wa dini	7-12-1965

Hati zote za Mtaguso zinapatikana katika tafsiri ya Kiswahili: HATI ZA MTAGUSO MKUU WA VATIKANO II – tafsiri ya Familia za Maamkio – ed. TEC – Baraza la Maaskofu Tanzania – Ndanda 2001 – ISBN 9976-63-649-0

Mapokezi ya mtaguso

Kwa kuwa Roho Mtakatifu alitaka hivyo, Wakristo walio wengi walipokea kazi ya mtaguso kwa mikono miwili, na wengi nje ya Kanisa pia waliridhika sana. Kutokana nao yamepatikana matunda mengi, lakini zimejitokeza hata kasoro na shida kwa sababu mbalimbali, hasa kwa kutoelewa wala kutotekeleza sawasawa maagizo yake. Kwa vyovyote hatuwezi kusema yote yaliyotokea baada ya mtaguso yamesababishwa nao, k.mf. maovu yaliyofanywa na baadhi ya mapadri hayamo kabisa.

Pamoja na upinzani wa wazi wa mifumo kadhaa ya kisiasa (ukomunisti na ubepari) na matapo mengine (Wamasoni n.k.) dhidi ya Kanisa, hali ya jumla ya ulimwengu inazidi kuelekea anasa na kuabudu utajiri hata kuzima maisha ya Kiroho. Hivyo ni vigumu kufanikisha mtaguso.

Hata ndani ya Kanisa wengi wamesoma hati zake kijuujuu, wakishikilia upande mmoja na kutojali wa pili. Wengine wamevunjika moyo kuona utekelezaji wa mtaguso unavyokwenda polepole. Wengine wameshughulikia miundo tu ya Kanisa, bila ya kujali fumbo la Kimungu lililomo ndani yake. Pengine umekosekana upambanuzi, k.mf. wengi walipofuata mitazamo ya ulimwengu uliomuasi Mungu badala ya kujadiliana nao ili kuuokoa.

Matatizo yaliyojitokeza baada ya mtaguso yanaonyesha haja ya kuupokea vizuri zaidi, kwa kupiga hatua nne zifuatazo:

1. Hati za mtaguso zijulikane na watu wengi zaidi na kwa dhati zaidi.
2. Zipokewe kwa moyo.
3. Zizingatiwe kwa upendo.
4. Zitekelezwe maishani.

Namna ya kuelewa mtaguso

Tukitaka kuelewa vizuri hati za mtaguso, ni lazima tuzizingatie zote 16 zilivyo na zinavyofungamana. Ni lazima pia tutie maanani hasa katiba zake 4, kwa kuwa ndizo hati kuu zinazotuwezesha kuelewa maagizo 9 na matamko 3. Tena hatutakiwi kutenganisha mtazamo wa kichungaji na msingi wa imani wa hati hizo, wala kutenganisha roho ya mtaguso na hati zenyewe. Mwishowe mtaguso ueleweke katika mapokeo ya Kanisa kwa kuwa katika mitaguso yote Kanisa ni lilelile. Hivyo tu tutapata mwanga tunaouhitaji kwa wakati huu.

Tahadhari hizo zote zinahitajika kwa sababu katika kutekeleza mtaguso yamejitokeza maelekeo mawili ambayo yanapingana na kuvuruga hali ya Kanisa. La kwanza linadai mabadiliko yasiyolingana na mtaguso, ingawa wenyewe wanasema ni maendeleo yanayotakiwa na roho ya mtaguso. Maendeleo ya namna hiyo hayakubaliki kwa sababu hayajali mapokeo ya mitume yanayodai imani idumu kuwa

ileile. La pili linaambatana na mambo ya zamani, bila ya kujali ishara za nyakati zetu zinazodai mambo mapya pia kwa wokovu wa watu wa leo na wa kesho.

Ni wajibu wa maaskofu chini ya Papa kutambua yapi yanajenga na yapi yanazuia ujenzi au pengine yanabomoa Kanisa. Ndiyo kazi inayofanyika hasa katika sinodi (= pamoja-njia, yaani kusafiri pamoja). Kati ya sinodi za ngazi mbalimbali kuanzia ile ya jimbo, muhimu zaidi ni zile za kimataifa zinazofanyika mara kwa mara huko Roma (mtaa wa Vatikano), zikikusanya maaskofu wawakilishi wa nchi zote na baadhi ya wakuu wa mashirika ya kitawa.

Juhudi za kutekeleza mtaguso

Kama vile mitaguso mikuu iliyotangulia kupanga urekebisho wa hali ya Kanisa, mtaguso wa pili wa Vatikano pia ujumbe wake hautaweza kuzaa matunda isipokuwa kwa juhudi za muda mrefu. Miaka ishirini baada ya mtaguso kumalizika, sinodi maalumu iliyoitishwa ili kutathmini matokeo yake ilisema wazi kuwa kazi bado sana, kwa namna ya pekee kuhusu kulenga utakatifu kwa waamini wote. Ndiyo maana ilihamasisha tufanye juu chini ili ujumbe wa mtaguso usikilizwe upya katika kila jimbo. Ni lazima tushike jembe kwa kazi hiyo bila ya kuangalia nyuma tukipatwa na matatizo yasiyoepukika.

Hati za mtaguso mojamoja

SACROSANCTUM CONCILIUM

Kikao cha pili cha mtaguso kilipitisha hati mbili za kwanza. Ya kwanza kabisa inahusu liturujia ambayo ni moyo wa Kanisa kwa kuwa ndipo linapoungana na Mungu wake na kuonekana katika sura yake takatifu. Lengo la hati hiyo ni kufanya kwanza mapadri, halafu Wakristo wengine pia waelewe na kutimiza liturujia ili kwa njia yake wamtukuze kweli Mungu na kufaidika Kiroho.

Karne ya XX iliiandaa kwa kuwa wataalamu walijitahidi kwa muda mrefu kuchambua maana ya liturujia kwa jumla na ya ibada zake mbalimbali. Mapapa wote walipokea na kuagiza marekebisho kadhaa yalitopendekezwa na wataalamu hao. Lakini kazi kubwa zaidi ilikuwa bado.

Kikwazo kikuu kilikuwa ni lugha ya Kilatini iliyokwishakufa tangu miaka elfu hivi. Muda huo wote wasomi tu waliweza kuelewa masomo na mengineyo ya liturujia. Hivyo watu wa kawaida wakawa watazamaji tu wa matendo ya ibada. Bila ya kupata mafundisho wala sakramenti ya ekaristi, Wakristo wa magharibi walijitungia ibada zao badala ya kutegemea liturujia ya Kanisa.

Huko mashariki hali ilikuwa tofauti kabisa: ndiyo sababu hati hiyo inahusu liturujia ya Roma tu, isipokuwa misingi ya liturujia yoyote na mengineyo yanayofaa hata mashariki.

Sura ya kwanza inahusu kanuni za jumla kwa urekebisho na ustawishaji wa liturujia. Kwanza inaeleza undani na umuhimu wake, halafu inasisitiza haja ya malezi ya kiliturujia kuanzia seminari na nyumba za kitawa ambapo maisha yote yafuate roho ya liturujia na masomo yote yafundishwe kwa kuonyesha uhusiano wake na liturujia ambayo ihesabiwe kati ya masomo muhimu zaidi na kufundishwa na wataalamu. Hivyo waamini wote watasaidiwa kuchota roho halisi ya Kikristo katika chemchemi hiyo ya kwanza na ya lazima; pia wataweza kushiriki ibada kwa jinsi iliyo haki na wajibu wao.

Baadaye tu yanaagizwa marekebisho ya jumla ya liturujia na vitabu vyake vyote; msingi wake ni kwamba liturujia, mbali ya mambo yaliyoagizwa na Bwana, ina mengi yaliyopangwa na Kanisa lenyewe katika historia yake kulingana na mahali na nyakati mbalimbali. Kwa hiyo mara kwa mara linaweza na kupaswa kuyapanga upya kwa manufaa ya waamini.

Kwa kuwa liturujia ni kazi ya Kanisa lote, inaratibiwa na uongozi wake tu: wengine wasithubutu kubadilisha lolote wanapofanya ibada zake. Hata uongozi wa Kanisa usirekebishe vitabu harakaharaka na pasipo lazima, bali uhakikishe kwamba mapya yanalingana na ya zamani.

Kwa namna ya pekee ni lazima neno la Mungu katika liturujia liheshimiwe linavyostahili, tena lionjwe kama ilivyokuwa mwanzoni mwa Kanisa.

Maagizo mengine yanatokana na hali ya kijumuia ya liturujia, yaani kwamba ibada zake si za binafsi, bali ni za Kanisa lote, na kila mmoja anahusika namna yake kama mwamini wa kawaida au kama mwenye daraja au huduma fulani. Hivyo ipendelewe ibada ya pamoja ambapo kila mmoja ashike nafasi yake na kulingana vizuri na wengine wanaoshika nafasi zao.

Maagizo mengine yanazingatia faida ya waamini upande wa imani ikiwa ni pamoja na kujifunza undani wa imani yenyewe. Kwa ajili hiyo mtaguso umeamua ibada zieleweke kwa urahisi, mapadri watoe hotuba na mawaidha mbalimbali wakati wa ibada, pia ziruhusiwe lugha hai za watu ingawa Kilatini kinabaki lugha rasmi ya madhehebu ya Kanisa la magharibi na waamini wake wote wanatarajiwa kujua kuitikia na kuimba kwa Kilatini wakati wa Misa.

Mbali ya lugha, mtaguso umekubali yafanyike marekebisho mengine ili kupokea katika liturujia ya Roma utamaduni wa makabila yoyote mradi usipingane na imani. Utamadunisho huo ufanyike chini ya Baraza la Maaskofu na kukubaliwa na Roma.

Mwisho wa sura hiyo unasisitiza umuhimu wa watu kushiriki liturujia ya askofu katika Kanisa kuu na ile ya parokia ili waamini wajisikie kweli Kanisa moja.

Ili kustawisha liturujia mtaguso umeagiza ziwepo kamati maalumu kitaifa na kijimbo.

Ili kutekeleza yaliyosemwa hapo juu*, sura ya pili* inaagiza namna ya kurekebisha madhehebu ya Misa, *sura ya tatu* inafanya vilevile kuhusu sakramenti nyingine na visakramenti, na *sura ya nne* kuhusu Sala ya Kanisa. Vitabu vyote vinavyohusika tunavyo tayari vimerekebishwa: katika kuvitumia ni muhimu kujisomea utangulizi wake.

Sura ya tano inarekebisha mwaka wa Kanisa kusudi mpango wake ueleweke zaidi bila ya kujaa mno sikukuu za watakatifu: hasa siku ya Bwana na vipindi maalumu vya mwaka vipate nafasi vinavyostahili.

Sura mbili za mwisho zinahusu muziki na sanaa takatifu ili liturujia ipendeze kwa uzuri wake, iinue roho kwa Mungu na kuwa kielelezo cha ile ya mbinguni. Hivyo vipawa mbalimbali vya binadamu vitumike kumtukuza Mungu. Hayo yameelezwa baada ya vitabu kwa sababu hivyo vina neno la Mungu na maitikio yetu kwa neno hilo lenye kututakasa. Vilevile muziki unaelezwa kabla ya sanaa nyingine kwa sababu unaambatana na maneno matakatifu. Mtaguso umesisitiza umuhimu wa kuimba katika liturujia, ukiagiza malezi kwa ajili hiyo, uundaji wa kwaya, utungaji wa nyimbo ambazo zichote hasa katika vitabu vya Biblia na liturujia. Kuhusu aina za muziki mtaguso umekubali aina yoyote inayoweza kulingana na utakatifu wa ibada; vilevile umeruhusu ala mbalimbali za kufaa. Hata hivyo liturujia ya Roma inapendelea muziki wa Kigregori na kinanda cha mabomba. Sanaa nyingine pia zinaheshimiwa na kutumiwa na Kanisa kwa ujenzi, mapambo, vifaa na picha takatifu. Kadiri ya mahali na nyakati limekubali mitindo mbalimbali mradi ilingane na imani, maadili na ibada ya Kikristo. Mtaguso umeagiza maaskofu hasa wajitahidi kudumisha msimamo huo na uzuri wa yote yanayohusu liturujia, kwa kuelimisha wanasanaa na makleri.

LUMEN GENTIUM

Hati hiyo juu ya Kanisa ndiyo muhimu kuliko nyingine zote za mtaguso. Inajibu swali la PauloVI, "Kanisa, unasemaje juu yako?".

Sura ya kwanza inafafanua fumbo la Kanisa ambalo, kama sakramenti, lina mawili yasiyotenganika: kwa nje linaonekana kwa namna fulani, na kwa ndani mwa neema isiyoonekana inayoletwa na yale yanayoonekana. Ndani ya Kanisa la watu Mungu anaishi na kufanya kazi.

Kwa hiyo hati inaanza kwa kueleza jinsi Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanavyohusika na Kanisa. Halafu unaonyesha kuwa Kanisa ni mwanzo wa ufalme wa Mungu, nalo linafananishwa na kundi la kondoo, shamba, jengo na hekalu la Mungu au bibiarusi anayeungana na Bwanaarusi wake kuwa mwili mmoja, yaani mwili wa Kristo: ndio ukweli wenyewe wa Kanisa.

Baada ya kuona ukweli huo wa ndani, *sura ya pili* inaelekea kutazama watu wanavyohusika na fumbo la Kanisa. Kuanzia Agano la Kale Mungu hakupenda kuokoa watu mmojammoja bali aliwaunganisha wawe taifa lake lenye kujua ukweli na kumtumikia kitakatifu. Katika taifa hilo wote wamejaliwa ukuhani ambao unatumika katika adhimisho la sakramenti, na unabii wenye karama mbalimbali.

Katika taifa hilo watu wote wanapaswa kuingia bila ya ubaguzi ili wawe kitu kimoja. Ndiyo maana ya jina "Katoliki": la mahali pote na nyakati zote. Wote wanahusiana na Kanisa ila kwa namna mbalimbali. Kwanza wapo Wakatoliki, yaani waliojiunga nalo kikamilifu kwa kumkubali Roho Mtakatifu na miundo yake yote. Halafu wapo Wakristo wengine waliokwishabatizwa na hivyo wameungana nalo ingawa si kikamilifu, kwa sababu hawakubali baadhi ya mafundisho na miundo yake. Hatimaye wapo watu wengine pia, wenye dini mbalimbali au wasio na dini, ambao wote wanaitwa na Mungu wajiunge na Kanisa kwa kuwa linahitajika kwa wokovu, ingawa Mungu anaweza kuwaokoa wenye nia njema wasiopata habari njema.

Bila ya shaka hali ya Wakatoliki ni bora zaidi, nao wanapaswa kuwashirikisha wengine wote ili kuwaokoa kutoka udanganyifu wa shetani na ulimwengu. Ndiyo maana ya kazi ya kimisionari ambayo imeagizwa na Yesu na ni wajibu wa kila Mkristo.

Sura ya tatu inatoa mafundisho muhimu tena mapya kuhusu muundo wa uongozi wa Kanisa, hasa uaskofu. Ni kwamba mtaguso wa I wa Vatikano ulifundisha sana kuhusu Papa lakini haukupata nafasi ya kutoa hati iliyopangwa juu ya maaskofu, kwa sababu ulisambaratika jeshi la Italia lilipoteka Roma. Hivyo mtaguso wa PILI wa Vatikano ulikusudia kukamilisha kazi hiyo.

Hasa umefundisha kwamba kama vile mitume walivyokuwa kundi moja na Petro na chini yake, maaskofu wote ni kundi moja na Papa wa Roma na chini yake. Kwa mpango wa Mungu kundi hilo ni la kudumu, maaskofu wakiwa waandamizi halisi wa mitume, na Papa mwandamizi halisi wa Petro, mkuu wao.

Kwa namna ya pekee mtaguso umefundisha kuwa ibada ya kumweka wakfu askofu ni ngazi ya juu kabisa ya sakramenti ya daraja, si baraka fulani kwa padri anayepewa kazi ya juu kama wengine walivyodhani awali. Hivyo uaskofu unatia alama isiyofutika milele. Kutokana na fundisho hilo, mtaguso umesisitiza kila mara umuhimu wa maaskofu katika maisha yote ya Kanisa.

Lakini mtaguso umesisitiza pia umoja wa maaskofu, ukidai kila mmoja wao afanye kazi yake akishirikiana na kundi lote na achangie ustawi wa Kanisa zima, si jimbo lake tu. Katika hilo askofu ndiye nguzo ya umoja wa waamini wake wao kwa wao tena kati yao na waamini wote duniani: hivyo linafanya listahili kuitwa Kanisa, kwa kuwa ndani yake Kanisa lote limo kweli. Kwa msingi huo askofu anawakilisha Kanisa lake maalumu katika Kanisa Katoliki, na kulifundisha, kulitakasa na kuliongoza kwa msaada wa mapadri wake na wa mashemasi, ambao wote wanashiriki ukuhani wake mkuu.

Mwishoni mwa sura hiyo Kanisa la magharibi linaruhusu ushemasi wa kudumu urudishwe na kutolewa kwa wanaume wenye ndoa pia.

Mara baada ya sura inayohusu wale wachache waliopata daraja takatifu (wanaoitwa makleri), inafuata *sura ya nne* juu ya Wakristo wa kawaida (wanaoitwa walei). Kwa karne nyingi hao walibaki kama wasikilizaji na watazamaji tu katika ibada na katika maisha yote ya Kanisa, lakini kuanzia karne ya XIX utume wao ulianza kuamka upya. Mtaguso umesisitiza kwa nguvu wajibu na haki yao ya kutumia neema na vipaji walivyojaliwa na Mungu kwa ujenzi wa taifa lake na kwa wokovu wa ulimwengu. Msingi wake ni ubatizo uliowafanya manabii, makuhani na wafalme; hivyo wamejaliwa huduma na karama mbalimbali ambazo wachungaji wanapaswa kuziheshimu wakiwaachia uhuru na nafasi katika utendaji. Kwa namna ya pekee ni juu yao kulenga utawala wa Mungu kwa kushughulikia malimwengu.

Baada ya kuona hayo makundi mawili ya waamini, wanaotofautiana kwa alama walizotiwa rohoni na ubatizo na kipaimara tu, au na daraja takatifu pia, *sura ya tano* inahusu wito unaowaunganisha wote, yaani kupata utakatifu. Karne za nyuma wengi walidhani hiyo ni kazi ya watawa tu, waliojichagulia "hali ya ukamilifu", au sanasana mapadri. Kumbe sivyo: Wakristo wote wanapaswa kulenga utakatifu, kila mmoja kadiri ya wito wake maalumu na hali yake maishani. Hati inaorodhesha aina mbalimbali za waamini na jinsi kila moja ilivyo na njia yake; halafu inakumbusha njia mbili bora, yaani kifodini na mashauri ya Kiinjili: kwa maisha na kifo chao mashahidi na watawa wanahimiza Wakristo wote kutafuta ukamilifu wa upendo.

Hivyo ni rahisi kuelewa kwa nini *sura ya sita* inazungumzia watawa. Hao hawahusiki na uongozi wa Kanisa (isipokuwa kama wamepata pia daraja takatifu), ili wanahusika moja kwa moja na utakatifu na uhai wake. Si kundi la tatu kati ya makleri na walei, bali ni walei au makleri waliojifunga kulenga utakatifu kwa kushika mashauri ya Kiinjili, yaani useja mtakatifu, ufukara na utiifu. Mtaguso umesisitiza umuhimu wa mtindo huo wa maisha na asili yake katika maneno na mifano ya Yesu: utawa hautokani na historia ya Kanisa tu, bali upo na lazima uwepo kwa mpango wa Mungu. Hivyo uongozi wa Kanisa unapaswa kuuratibu na kuudumisha katika mitindo yake mingi. Mtawa amewekwa wakfu kwa ubatizo, halafu anaimarisha hali hiyo kwa nadhiri ili achume kwa wingi zaidi matunda ya neema kwa kuondoa mapingamizi yoyote yanayoweza kumzuia maishani.

Baada ya kuwaongelea watawa, wanaoshuhudia kwa namna ya pekee ulimwengu mpya ambapo hapana ndoa, *sura ya saba* inakuja kufundisha kuwa Kanisa lote hapa duniani liko safarini kuelekea mbinguni, huku likiwa na umoja na watakatifu. Sura hiyo inasisitiza tena imani yetu kuhusu mambo ya mwisho ikituhimiza tutazame juu na pia tuzingatie mifano bora ya wale waliokwishafikia heri ya milele. Hao wanastahili tuwaheshimu na kuwaomba watuombee, mradi tuepuke makosa mbalimbali yaliyojitokeza huku na huku. Daima ionekane wazi kuwa tunamuabudu Mungu tu na kwamba tukiwaheshimu watakatifu ni kwa sababu ni marafiki wa Mungu na wafuasi hodari wa Mwanae. Tunawaheshimu sio tu ili kupata msaada fulani, bali hasa kwa kufuata mifano yao ili tuwafikie katika liturujia ya mbinguni kuwaabudu Mungu na Mwanakondoo.

Mwishoni mwa hati hii yanapatikana mafundisho kuhusu Bikira Maria, akiwa ni mkuu wa watakatifu na mfano wa Kanisa lote. Baada ya mabishano makali kati ya washiriki wa mtaguso, wingi wa kura ulikataa kutoa hati maalumu juu ya Maria peke yake, kwa kuwa hawezi kueleweka nje ya fumbo la Kristo na la Kanisa. Hivyo mafundisho hayo yamepangwa katika *sura ya nane* ya hati hii, si kwa nia ya kuamua mabishano kati ya wanateolojia, wala kufundisha mapya, bali kupanga upya mafundisho ya Maandiko na ya Mapokeo. Baada ya kumsifu sana Bikira, mtaguso umesisitiza juu yake pia kuwa Kristo ndiye mshenga pekee kati ya Mungu na watu, hivyo hatuwezi kumlinganisha Maria na yeye kama walivyowahi kufanya baadhi ya waamini. Mchango wake kwa ukombozi wetu ulitokana na ukombozi ulioletwa na Yesu, ni kushiriki kazi yake tu. Hivyo Maria azidi kuigwa na kuheshimiwa kwa namna ya pekee, hasa kwa njia ya liturujia, lakini kwa kukwepa neno lolote ambalo linapita kiasi au kumweka pembeni Kristo.

Wazo kuu la hati hii kuhusu Kanisa ni kwamba lenyewe hasa ni ushirika wa Mungu nafsi tatu na watu, ni ushirika wa watakatifu wa duniani, toharani na mbinguni, ni ushirika wa waamini wa aina mbalimbali, kama vile wenye daraja na walei, au watawa na wenzao wote. Ushirika huo unatakiwa kuonekana wazi katika maisha ya Kanisa katika ngazi zote; hivyo litaonekana lilivyo, yaani ishara na chombo cha kuwaunganisha watu wote katika umoja wa Utatu mtakatifu.

DEI VERBUM

Katika Kanisa Katoliki tangu zamani sana zilisisitizwa liturujia na sakramenti, ingawa lugha ya kawaida ilikuwa haitumiki katika ibada hizo. Hivyo waamini walikuwa hawaelewi masomo ya Biblia wala matini mengine. Kwa jumla walikuwa hawaelewi Neno la Mungu kwa kukosa tafsiri za vitabu vyake hata nyumbani. Kuanzia karne ya kumi na mbili tafsiri hizo zilianza kupatikana kwa juhudi za wazushi waliozitumia kupinga ualimu wa Kanisa. Baadaye watu walipobuni uchapishaji, kitabu cha kwanza kutolewa kikawa ni Biblia huko Ujerumani. Mara ukaanza Uprotestanti pia ambao katika madhehebu yake yote ulisisitiza Maandiko kwa kukataa Mapokeo na Ualimu wa Kanisa. Ndiyo sababu yenyewe yalifanya kazi kubwa ya kutafsiri na kueneza Biblia ulimwenguni kote. Upande wake Kanisa Katoliki likaogopa kwa kuona nchi ngapi zimeliasi, hivyo likachukua msimamo wa kinyume kwa kusisitiza tena Mapokeo na Ualimu wake. Basi, Biblia ikazidi kubaki pembeni mwa maisha ya Wakatoliki wengi. Hata mwanzoni mwa karne ya XX walipojitokeza wataalamu wa Biblia walikatazwa wasifundishe baadhi ya mambo mapya kuhusu utungaji na maana ya Maandiko. Hivyo kabla ya mtaguso Wakatoliki kwa jumla walikuwa wakiogopa Biblia badala ya kuipenda.

Kumbe hati hiyo kuhusu ufunuo wa Kimungu ilipotolewa baada ya majadiliano na marekebisho mengi imelirudishia Kanisa lote Maandiko Matakatifu. Hapo Wakatoliki wataalamu wa Biblia wamefanya kazi kubwa sawa na wenzao Waprotestanti. Waseminari na watawa wengi wamefundishwa sana Neno la Mungu, na hata walei wameanza kulifurahia. Matunda yake yamepatikana tayari katika uzima mpya unaoonekana katika mifumo ya Kiroho, vyama na jumuia mbalimbali.

Baada ya *dibaji,* inayotamka nia ya kufuata nyayo za mitaguso iliyotangulia, *sura ya kwanza* inahusu ufunuo wa Mungu. Ni kwamba hatuwezi kuelewa Biblia mbali na historia ya wokovu, kwa sababu si kitabu kilichoandikwa leo kwa ajili yangu mimi, bali kilipatikana zamani Mungu alipojifunua hatua kwa hatua.

Sura ya pili inafundisha jinsi ufunuo huo uliokamilika zamani za Yesu unavyotufikia sisi watu wa leo, yaani kwa njia ya Mapokeo ya Mitume yakiwa na Maandiko Matakatifu ambayo kwa pamoja ni hazina takatifu ya Neno la Mungu, si chemchemi mbili tofauti. Hazina hiyo imekabidhiwa kwa Kanisa ambalo linaweza kuifafanua rasmi kwa njia ya Ualimu wake. Basi, Mapokeo Matakatifu, Maandiko Matakatifu na Ualimu wa Kanisa yameshikamana na kuunganika kiasi kwamba moja haliwezi kusimama bila ya mengine.

Baada tu ya kuelewa hayo tunaweza kukabili Biblia yenyewe *(sura ya tatu)* kwa kuzingatia jinsi Roho Mtakatifu alivyovuviwa juu ya waandishi wake. Hao walifanya kazi kama waandishi wowote, lakini vitabu vilivyopatikana vinafundisha tu kwa hakika na bila ya kosa ule ukweli ambao Mungu alitaka uandikwe kwa wokovu wetu. Si ukweli wowote (k.mf. wa sayansi) bali ule unaohusu wokovu. Hivyo Biblia mwandishi wake hasa ni Mungu, lakini yeye alijieleza kwa njia ya watu tena kwa namna ya kibinadamu. Basi, tukitaka kumuelewa tunapaswa kuelewa kwanza waandishi walitaka kusema nini tukizingatia pia mitindo waliyoitumia. Utaalamu huo ni muhimu ingawa hautoshi, kwa sababu tunapaswa bado kuzingatia umoja wa Biblia nzima, Mapokeo ya Kanisa na kweli za imani.

Baada ya kuona habari za Biblia kwa jumla, *sura ya nne* inaeleza umuhimu wa Agano la Kale kwa Wakristo pia, kwa kuwa linashikamana na Agano Jipya kama kitabu kimoja ambacho pande zake mbili zinahitajiana.

Sura ya tano inaeleza juu ya Agano Jipya: kwanza ubora wake unaozidi vitabu vya kale; halafu asili ya Kitume ya Injili nne ambazo tena zinapita hata Maandiko mengine ya Agano Jipya; mwishowe hakika ya kihistoria ya Injili hizo. Hati hii imepokea pia mtazamo mpya uliosema Wainjili waliandika historia ya Yesu kwa kuchagua baadhi ya habari, kufupisha nyingine na kueleza upya nyingine kadiri ya mazingira, wakidumisha namna ya kuhubiri kwa lengo la kufanya watu waamini. Habari zenyewe ziliwaelea kwa mwanga wa Roho Mtakatifu aliyelifikia Kanisa baada ya Kristo kufufuka ili kuliongoza kwenye ukweli wote.

Hatimaye *sura ya sita* inatoa maagizo kuhusu Maandiko Matakatifu katika maisha ya Kanisa. Kwanza ziwepo juhudi mpya ili wote wapate lishe katika meza ya Neno la Mungu ambalo ni hai na lina nguvu. Pia juhudi zifanyike ili waamini wapate Maandiko hayo katika lugha zao. Wataalamu pamoja na kuyatafsiri wayafafanue na kuelimisha wengine. Wale wote wanaotoa mafundisho ya imani katika ngazi zozote washikamane na Maandiko kwa kuyasoma pamoja na kusali ili Biblia iwe kiini cha mafundisho yao. Waamini wote, hasa watawa, wanahimizwa kuisoma sana kwa sababu kutoijua ni sawa na kutomfahamu Kristo.

GAUDIUM ET SPES

Hati hiyo, ndefu kuliko zote za mtaguso, inaitwa ya kichungaji kwa sababu inataka kutazama mambo kwa lengo la kuongoza maisha ya watu. Sehemu yake ya kwanza inaweka misingi juu ya imani, na sehemu ya pili inaonyesha msimamo wa Kanisa kuhusu ulimwengu wa leo. Kichwa kinasema wazi kuwa hati inahusu Kanisa katika ulimwengu “wa kisasa”, kwa kuwa tunapaswa daima kuishi na

kutenda "leo", huku tukijua vizuri mambo yalivyo, tukitambua ishara za nyakati zijazo ili tuone njia za kufaa kwa wokovu wa ulimwengu.

Bila ya shaka imepita miaka mingi tangu hati iandikwe, hivyo yameshatokea mabadiliko mengi, yaliyochunguzwa na mapapa na sinodi mbalimbali. Ingawa baadhi ya mambo leo yanaonekana tofauti kidogo, hati hiyo inabaki muhimu: kwanza kwa mtazamo wake wa jumla, pili kwa mtindo wa kuwaelekeza watu katika mambo ya kawaida yanayowahusu maishani, tatu kwa mafundisho ya msingi yasiyoweza kubadilika, nne kwa kuwa misimamo mbalimbali inafaa mpaka leo.

Kanisa halijioni tena mbali na ulimwengu, wala dhidi ya ulimwengu, bali ndani ya ulimwengu. Wakristo wanasafiri duniani pamoja na binadamu wenzao, wakishirikiana nao katika yale yote yasiyopingana na imani na maadili ya Kikristo. Hasa walei, ambao idadi yao ni karibu sawa na idadi ya wanakanisa wote, wanapaswa kuishi ulimwenguni kama chachu mpaka donge lote liumuke. Basi, Kanisa linajisikia kuhusika kabisa na maisha ya watu wote, hasa fukara. Ndiyo maana maneno ya kwanza ya hati hiyo yanasema kuwa "furaha na matumaini, huzuni na mafadhaiko ya watu ni pia ya wanafunzi ya Kristo".

Hati hiyo ni ujumbe wa Kanisa kwa watu wote unaotaka kuwasaidia waelewe mambo yanayotukia siku hizi, kwa kuwa katika hayo binadamu anaweza kujipatia maisha bora kweli na halafu uzima wa milele, au kinyume chake anaweza kudanganyika na kupotoka. Siku hizi ugumu wa pekee kwa binadamu ni kwamba mabadiliko ya kila aina yanatokea haraka ajabu, tofauti na zamani. Mtu wa kawaida hapati nafasi ya kuyafikiria kwa dhati na kuyachambua. Hivyo hatari yake ni kufuata mkondo au kuongozwa na matukio badala ya kujifanyia mpango wa kumfaa, hata anaweza akafikia hatua ya kushindwa kujielewa ni nani, pamoja na kukosa msimamo maishani na raha moyoni mwake. Basi, anahitaji kuchungwa na kuelekezwa kwa imani na upendo: ndiyo kazi ya Kanisa ambalo lina nafasi nzuri ya kuwatangazia watu majibu ya Injili kwa maswali yanayowakera.

Kwa ajili hiyo hati inamuongoza msomaji hatua kwa hatua kufikiria utatanishi wa kisasa katika nadharia, jamii, uchumi na siasa unaomfanya afadhaike, hasa akiona maendeleo hayafaidishi wote na pengine yanatumika dhidi ya binadamu. Hivyo anaweza kutambua kuwa shida zinaanza moyoni mwake, ambamo mna mashindano makali na maswali ya msingi kama vile, "Mtu ni nani? Mateso na kifo vinavyodumu hata wakati huu wa maendeleo makubwa maana yake nini? Mtu ailetee nini jamii na atarajie kupata nini toka kwake? Baada ya maisha haya kutakuwa na nini?". Jibu ni Kristo, mwokozi pekee, kiini na lengo la historia yote, msingi hasa usiobadilika. Katika mwanga wake mtaguso umechunguza fumbo la binadamu na wito wake.

Katika sehemu ya kwanza, sura ya kwanza inaeleza hadhi ya binadamu yeyote. Ingawa karibu wote wanakubali kuwa mtu ni kiumbe bora duniani, Kanisa linasisitiza ukweli huo kwa kumuona na kumuita "sura ya Mungu" hata baada ya kuathiriwa na dhambi. Ndio msingi wa heshima anayostahili katika mwili na zaidi katika roho ambayo kwa akili inaweza kujipatia ukweli na hekima, kwa dhamiri inasikia wito wa Mungu, na kwa hiari inaweza kuuitikia. Lakini Kanisa, pamoja na kusisitiza hiari kama wanavyofanya wengi siku hizi, linahimiza pia kuitumia vizuri, kwa kuwa mwishoni kila mtu atahukumiwa juu ya matumizi ya vipawa vyake.

Baada ya kukabili swala la kifo kwa kutangaza habari njema ya ufufuko, hati inakabili janga mojawapo la siku hizi, yaani kwamba wengi wanakanusha uwepo wa Mungu au wanaishi bila ya kumjali. Mtaguso ulifikiria hasa ukomunisti na misimamo mingine ya kupinga na kuzuia dini zote, lakini badala ya kuilaani tu, umetuhimiza kujadiliana na kushirikiana nayo, pamoja na kutoa ushuhuda wa maisha bora ya Kikristo, ukikiri kuwa pengine mifano yetu mibaya ndiyo iliyosababisha wengi wakose imani. Mwisho inachorwa taswira ya Kristo, mtu mpya, ambaye pekee yake anaangaza fumbo la binadamu pamoja na uchungu na kifo.

Sura ya pili inatupatia mafundisho kuhusu jamii yanayozingatia mpango wa Mungu wa kuwa watu waishi kwa ushirikiano. Kuukamilisha ushirikiano huo kwa msingi wa haki ni muhimu kuliko maendeleo ya ufundi tu. Kwa ajili hiyo kila mtu awajibike kuhusu wenzake wote bila ya kumsahau hata mmoja, akijifanya jirani wa wenye shida na kujitahidi kustawisha usawa kwa kutumia nafasi yoyote aliyonayo katika jamii. Maadili ya kibinafsi hayakubaliki, bali wajibu mkuu mmojawapo ni kujihusisha na ustawi wa jamii na mshikamano ili wote kwa neema ya Kristo waishi kijamaa.

Sura ya tatu inatoa msimamo kuhusu utendaji wa binadamu ulimwenguni. Hasa leo ambapo maendeleo ni ya haraka tunajiuliza kuhusu maana ya juhudi zetu na namna ya kuziendeleza. Ni hakika kuwa Mungu ametuagiza tufanye kazi na kutawala ulimwengu ili wote wapate hali ya maisha wanayostahili walio sura yake. Wakristo wanapaswa kuwa mstari wa mbele bila ya kudhani eti, Mungu anauonea kijicho ushindi wowote wa binadamu juu ya maadui wake (ujinga, maradhi na ufukara). Kinyume chake ushindi huo unatangaza ukuu wa Mungu aliyemuumba mtu akiwa na akili nyingi.

Lakini binadamu asisahau kuwa ubora wake hautokani na wingi wa vitu anavyojipatia, bali unategemea tuni za kiadili anazostawisha kwa kazi yake, hasa haki na udugu. Shida ni kwamba mara nyingi akishindwa na dhambi anafuata ubinafsi au utaifa na kuanzisha miundo ya dhuluma na vita hata kutengeneza silaha za kutosha kuangamizia uhai wowote duniani. Mbele ya hali hiyo Wakristo wanapaswa kutofuata mitindo ya ulimwengu bali njia ya upendo nyuma ya Kristo, wakiwa tayari kubeba msalaba wanaotwishwa wale wanaotafuta haki na amani. Tumaini la uzima wa milele

lisipunguze bidii yetu kwa maisha ya binadamu wa leo, kwa kuwa huyo anaandaliwa hapa duniani kuingia katika ufalme wa mbinguni.

Katika utendaji wake mtu ana haki ya kufuata taratibu za elimudunia , siasa n.k. Imani haiogopi kumuachia nafasi hiyo, kwa kuwa Mungu yuleyule aliyejifunua kwetu kwa imani ameumba pia vitu vyote na kutujalia akili na uvumbuzi. Mtaguso umelaumu mawazo finyu yanayogonganisha imani na sayansi.

Sura ya nne inaeleza yatokanayo na zile zilizotangulia, yaani uhusiano wa Kanisa na ulimwengu. Kanisa likiwa na lengo la milele, linaishi duniani na wanae ni pia raia wa nchi hii. Hivyo linachangia ustawi wa binadamu pamoja na kupokea kwa shukrani misaada mbalimbali ya walimwengu. Lina ujumbe kwa watu wote kuhusu wokovu, lakini pia kuhusu maisha haya, hasa hadhi na haki za kila mtu. Kwa hiyo, ingawa utume wa Kanisa ni wa kidini hasa, linashughulikia pia ustawi wa jamii na umoja wa mataifa. Wakristo wasisahau tena majukumu yao ya kidunia, wala wasiyaone hayahusiki na imani. Mojawapo kati ya makwazo makubwa zaidi ya nyakati zetu ni utengano huo kati ya imani na maisha ya Wakristo wengi. Kwa namna ya pekee, walei wanapaswa kushughulikia malimwengu yote kwa mfano wa Yesu huko Nazareti. Wasisubiri kuagizwa na wachungaji wao, kwa kuwa kuratibu hayo ni kazi yao hasa. Mtaguso umekiri tena ukosefu wa wanakanisa na kuwahimiza kujirekebisha wasije wakazuie uenezaji wa Injili. Vilevile umeshukuru kwa juhudi za watu wowote kwa ajili ya ustawi wa familia, utamaduni, uchumi, jamii, amani na mshikamano wa kimataifa, hata ukakiri Kanisa limefaidika sana na upinzani na dhuluma za maadui wake.

Baada ya kumaliza kueleza kwa jumla jinsi Kanisa linavyohusika na wito wa binadamu, hati hii katika *sehemu ya pili* inakabili maswala kadhaa yaliyo muhimu zaidi kwa watu wa leo.

Kati ya hayo *sura ya kwanza* inafafanua kwanza hadhi ya ndoa na familia na namna ya kuzipa nafasi za kufaa, kwa sababu mengine mengi yanategemea hali ya familia. Baada ya kueleza utakatifu wa ndoa, kwa kuifananisha na hali ya kuwekwa wakfu kwa njia ya sakramenti za kudumu, mtaguso umeonyesha ubora wa upendo kati ya mume na mke na namna ya kuutekeleza, ukisisitiza unavyoelekea uzazi. Hivyo watu wa ndoa wanapaswa kupanga kwa pamoja mbele ya Mungu na kwa kuzingatia mafundisho ya Kanisa ili wazae kwa busara na ukarimu. Kwa namna ya pekee inasisitizwa kuwa ni lazima uhai wa binadamu kisha kuanza ulindwe kwa bidii zote: kuua mimba au mtoto ni maovu ya kutisha. Katika magumu yanayohusu uzazi wa mpango, wanandoa wajitahidi kufuata usafi wa moyo unaowafaa. Hata jamii nzima inatakiwa kuchangia ustawi wa familia: viongozi watunge sheria na kufanya mipango kwa ajili hiyo; wanasayansi waendelee kutafuta njia halali za kupanga uzazi; mapadri wafanye juu chini familia ziishe kwa utulivu.

Sura ya pili inafikiria namna za kustawisha utamaduni, yaani zile namna maalumu ambazo binadamu anakabili maisha katika mazingira na nyakati mbalimbali kulingana na orodha ya tunu anazothamini. Tofauti na wanyama, yeye hawezi kufikia hali ya maisha ya kumfaa kweli asipoyafanyia kazi mema yaliyoumbwa na Mungu ndani mwake na kandokando yake. Kila kabila na kundi la watu lina utajiri wake ambamo binadamu achote ili kujiendeleza na kuwaendeleza wenzake.

Lakini huu wa leo ni wakati mpya wa historia kwa sababu ya mabadiliko ya haraka mno. Upande mmoja zimefunguliwa njia mpya za kukuza na kueneza elimu na za kuunganisha aina tofauti za utamaduni. Upande mwingine kuna hatari za kufuta hekima na sura maalumu za kila jamii, kuvuruga mafungamano kati ya vizazi, kuacha elimu ya juu mikononi mwa wataalamu tu n.k.

Kufuatana na amri ya upendo Wakristo wanatakiwa kuchangia na wenzao ujenzi wa ulimwengu ili wote waone vizuri kazi ya Mungu na namna ya kuiendeleza. Kama vile yeye alivyotumia utamaduni wa watu ajifunue kwao, ndivyo Kanisa pia lilivyofanya na linavyopaswa kufanya katika kueneza habari njema. Lenyewe limetumwa kwa mataifa yote, hivyo halibanwi na utamaduni wowote, bali linautumia na kuuchangia, linausafisha na kuuinua lisiishie ndani yake. Ni wajibu wa wote kujitahidi kufuta ujinga kwa kueneza elimu hasa ya msingi ili kila mtu aweze kuchangia zaidi ustawi wa jamii. Vilevile kila mtu aelewe wajibu wa kujiendeleza kiutu na Kiroho bila ya kutawaliwa na kazi za mikono tu, akitumia vitabu na vyombo vingine vya upashanaji habari, muda huru ulio nje ya kazi n.k.

Sura ya tatu inafundisha kuhusu maisha ya kiuchumi na ya kijamii ya mtu wa nyakati zetu. Ni lazima huyo awekwe juu kabisa kuliko maendeleo ya vitu, kwa kuwa ndiye mtendaji, kiini na lengo la uchumi na la jamii. Kumbe wengi wanazingatia sheria za uchumi tu ili kutajirika iwezekanavyo. Matokeo ni kwamba mtengo kati ya mataifa, na kati ya matabaka ndani ya nchi, unazidi kuwa mkubwa. Anasa za wachache zinaleta ufukara wa kutisha wa umati hata kuhatarisha amani duniani.

Binadamu wa leo anaweza kurekebisha hali hiyo, lakini yanahitajika mageuzi mengi katika mitazamo, mazoea na miundo pia. Hapo tu ongezeko la uzalishaji litasaidia kweli, yaani litamsaidia mtu yeyote katika mahitaji yake yote (ya mwili, ya nafsi na ya roho). Kwa ajili hiyo ni lazima uchumi usiachwe uende zake wala usitawaliwe na wachache, bali wote waweze kuuchangia ustawi na uongozi wake bila ya ubaguzi, wakisaidiwa kushika nafasi yao hasa kwa njia ya ustadi. Kazi ya binadamu iheshimiwe kuliko mengine yanayohusu uchumi (k.mf. mtaji au malighafi). Wote wana wajibu na haki ya kufanya kazi na kujipatia hivyo riziki za kutosha. Vilevile wana haki ya kupata muda kwa maisha ya

kifamilia, hasa akina mama. Wafanyakazi ni haki yao kuchangia uongozi wa kampuni, na vilevile kuunda vyama vya kutetea haki zao hata kwa migomo.

Mojawapo kati ya mambo yaliyozingatiwa zaidi na mtaguso ni njaa ya umati; kwa ajili hiyo umekumbusha kuwa Mungu ameumba vyote kwa ajili ya wote, basi ni lazima mali zigawiwe kwa haki na upendo. Ingawa mtu yeyote ana haki ya kumiliki vitu kadhaa, ni lazima kila mmoja awe na mali za kutosha, wasiwepo wenye kujipatia mali nyingi kiasi cha kuacha wengine wakose hata mahitaji. Matajiri wawajibike haraka kuwashirikisha wengine, la sivyo watakuwa wauaji wa wenye njaa. Hao wa mwisho ni haki yao kujipatia riziki kutoka utajiri wa wenzao. Kadiri ya mazingira tunaweza kuwa na njia mbalimbali za kuhakikisha wote wapate riziki zao (desturi za ukarimu, pensheni n.k.). Mashamba yagawiwe kwa wakulima wasiyonayo.Pesa zitumike ili kuandaa nafasi za kazi kwa watu wa leo na wa kesho wa nchi zote (vitegauchumi). Wakristo watafute ufalme wa Mungu hata katika uchumi na shughuli nyingine za kijamii.

Sura ya nne inafikiria siasa ambayo pia siku hizi inapitia mageuzi makubwa. Mchango wa Kanisa ni kutetea heshima ya kila mtu kwa kusisitiza kwamba lengo la siasa ni ustawi wa jamii nzima kuanzia watu na familia. Uongozi unahitajika ili kulinganisha kwa haki madai ya watu mbalimbali. Wananchi wote waelimishwe kuhusu siasa ili watoe mchango wao kwa kutumia nafasi wanazopewa (kura n.k.) na kwa kutetea haki zao bila ya kuwadai mno viongozi. Jamii na Kanisa vinawahudumia watu walewale lakini kwa namna tofauti, hivyo havichanganyikani bali ni vema vishirikiane. Hata hivyo Kanisa halifungamani na siasa yoyote, liweze kutangaza kwa uhuru maadili yanayotakiwa hata katika siasa, likipima mambo yote na kuhimiza yaliyo mema.

Hatimaye, *sura ya tano* inaongelea ujenzi wa amani na umoja kati ya mataifa. Wakati ilipoandikwa ulikuwa wa mafadhaiko makubwa kuhusu dunia nzima kuja kuangamizwa na wingi na ukali wa silaha zilizotengenezwa. Kwa msingi huo swala la vita linatakiwa tulifikirie upya kabisa, tusiridhike na msimamo wa zamani kuhusu masharti ya uhalali wake. Vilevile Wakristo wa madhehebu yoyote tuungane kati yetu, tena na wote wenye mapenzi mema, katika kujenga amani na haki. Kwa kuwa amani ya kweli sio tu kusimama kwa vita, labda kwa hofu tu ya silaha zilizolundikana; amani ni tunda la haki ambayo itafutwe mfululizo kwa bidii, tena ni tunda la upendo ule wenye msingi ndani ya Mungu. Kuhusu vita vinavyoendelea huku na huku, kwanza ukatili wake upunguzwe (kumbe siku hizi umezidi kwa sababu ya silaha mpya, mashambulizi ya raia, uangamizaji wa kabila zima n.k.). Utiifu kwa maagizo hauwezi kuwa kisingizio cha kutenda maovu, bali ni wajibu kuyakataa. Mapatano ya kimataifa kuhusu vita yaheshimiwe na wote. Ni wajibu wa viongozi wa nchi kuzilinda hata kijeshi, lakini wasitumie jeshi ili kugandamiza wengine. Pia waheshimu dhamiri ya wasiojisikia kutumia silaha. Vitendo vinavyowezekana leo vya kuangamiza miji mizima au maeneo mapana pamoja na wote waliopo ni makosa ya jinai yasiyovumilika. Wanaotengeneza au kununua silaha ili kujikinga na maadui wasije wakashambuliwa, wafikirie hatari ya silaha hizo kuja kutumika kweli, tena hasara ya maskini wanaokosa misaada wanayostahili kwa sababu tu pesa nyingi sana zinatumika kwa silaha. Tutafute mapema njia za upatanisho na muundo wa kimataifa wenye uwezo wa kudumisha amani na haki kwa wote. Hapo katikati akiba za silaha zipunguzwe kwa mpango wa pamoja. Viongozi na watu wao waache utaifa na misimamo yo yote inayotenganisha watu. Hasa malezi ya vijana na upashanaji habari vieneze mawazo ya amani na mitazamo mipana yenye faida kwa binadamu wote. La sivyo tutafikia tu ile amani ya kutisha itakayopatikana kwa kufa wote. Kanisa likisema hivi haliachi kutumaini na kuhimiza wongofu wa mioyo.

Kuhusu kujenga umoja kati ya mataifa, mara nyingi misingi ya kutoelewana ni hali tofauti mno za uchumi, nia ya kutawala, dharau ya wengine na vilema mbalimbali. Basi, ushirikiano mkubwa unaowezekana leo uwe njia ya kutatua matatizo hayo na kukidhi mahitaji ya watu, hasa maskini. Miundo ya kimataifa iliyopo iwajibike kuzingatia zaidi nchi zinazoendelea, wakimbizi na wengine wenye shida maalumu.

Ingawa miaka ileile ya mtaguso nchi nyingi zilipata uhuru wa kisiasa, hali ya uchumi inazirudisha chini ya ukoloni wa namna mpya. Basi, mshikamano uendeleze kweli nchi hizo. Lakini maendeleo yanategemea watu kuliko pesa, kwa hiyo kazi ya kwanza ni kuandaa raia wa nchi maskini kwa elimu na ufundi. Inahitajika misaada, mikopo na vitegauchumi tena kwa ukarimu, lakini pia kurekebisha sana sheria za uchumi wa kimataifa. Upande wao viongozi wa nchi maskini wapokee misaada hiyo kwa uaminifu, na raia wao wajitahidi kutumia vile vyote walivyo navyo. Maendeleo ya uchumi yasitusahaulishe roho ya binadamu, kwa kuwa huyo haishi kwa mkate tu.

Wengi leo wanafadhaishwa na kasi ya ongezeko la watu. Utatuzi wa kwanza ni kuleta usawa mkubwa zaidi kati ya watu na kueneza ujuzi kuhusu kilimo n.k. Halafu zitungwe sheria zinazosaidia familia, izuiwe kasi ya watu kuhamia mijini, watu waelimishwe kwa ukweli kuhusu hali ya nchi na uzazi wa mpango. Wote wajiepushe na njia za mkato zinazokwenda kinyume cha maadili na cha haki ya msingi ya wananchi kufunga ndoa na kuzaa wanavyoona vema wenyewe. Basi, wasaidiwe kuunda dhamiri na kujifunza njia halali za kupanga uzazi.

Wakristo wawe mstari wa mbele katika mshikamano wa kimataifa, wakijua Yesu katika maskini analia na kudai upendo. Mtaguso uliita kikwazo kuona nchi za Kikristo zikitapanya mali, wakati nyingine zinalemewa na njaa, maradhi n.k. Wakristo wajitolee kuhamia kwenye shida ili kusaidia kwa hali na mali wakishirikiana na miundo na watu wowote, kwa kuwa tunaye Baba mmoja na tunapaswa

kuishi wote kidugu. Hapo watatambulikana kama wafuasi halisi wa Kristo. Tukikumbuka kuwa hatutaingia mbinguni kwa kusema tu, Bwana, Bwana, bali kwa kutimiza mapenzi ya Baba, tukabili kazi hiyo kubwa ambayo tutahukumiwa siku ya mwisho kwa jinsi tulivyoifanya.

INTER MIRIFICA

Hati hiyo ilitolewa na mtaguso mapema ili kukabili jambo ambalo siku hizi ni zito sana kwa jinsi linavyochangia maisha na utamaduni wa watu duniani kote, yaani vyombo vya upashanaji habari. Hivyo vimeendelea hasa katika karne ya XX na kuwafikia karibu watu wote vikieneza habari, mawazo, maadili n.k. Kanisa linavipokea kwa shukrani kwa Mungu aliyempa binadamu akili ya kuvumbua na kubuni njia hizo zinazoweza kumuinua hata kidini. Lakini kwa ubaya wa moyo wake anaweza pia kuzitumia kwa uharibifu wake na wa wengine wengi, hasa watoto na vijana wasio na kinga. Kwa hiyo Kanisa linapaswa kushughulika ili vyombo hivyo vyote vitumike vema kwa kueneza habari njema, maadili na taarifa za kweli ili watu wakabili maisha vizuri na kuokoka. Pia liwaelimishe wote kuhusu namna ya kuchuja na kutumia vilivyo magazeti, vitabu, filamu, redio, televisheni n.k., wakielewa urahisi wa kudanganywa na kupotoshwa na vyombo hivyo. Hiyo ni kazi ya wachungaji, wazazi na walezi, lakini serikali pia isaidie kutunza mazingira safi. Mtaguso umeagiza shughuli hizo ziratibiwe kijimbo, kitaifa hata kimataifa. Kwa kuwa shughuli hizo zina gharama kubwa, Wakristo wanahimizwa kujitolea kwa ukarimu hasa Jumapili maalumu moja kwa mwaka.

ORIENTALIUM ECCLESIARUM

Mtaguso ulizingatia hali duni ya Makanisa Katoliki ya mashariki ukaamua kuirekebisha. Kwanza ulitamka kuwa yanastahili kuheshimiwa sana pamoja na mambo yote (liturujia, teolojia, sheria, miundo n.k.) kama sehemu ya hazina ya Kimungu iliyokabidhiwa kwa Kanisa. Liturujia zitunzwe kiaminifu na kurekebishwa kama zimeachana na mapokeo ya mashariki, hasa sakramenti zirudi kufuata taratibu asili. Mashirika ya Kilatini yajitahidi kuanzisha jumuia za mashariki. Madhehebu yoyote ya Kikatoliki yana haki na wajibu sawa hata kuhusu uenezaji Injili duniani kote. Wachungaji wa hayo yote wazoee kushirikiana, na wanaojiandaa kupata upadri waelimishwe juu ya uhusiano kati ya madhehebu hayo. Waamini wa mashariki wapatiwe mapadri na maaskofu wao popote wanapohitaji. Waortodoksi wakijiunga na Kanisa Katoliki waendelee kufuata madhehebu yao, na wenye daraja kati yao waendelee kuitumia. Kutokana na umuhimu wa patriarki kwao, hadhi na haki zake zirudishwe kama kabla ya utengano na Waortodoksi, na Makanisa yasiyo naye yafikiriwe. Hatimaye hati hiyo inahimiza Wakatoliki wa mashariki kushughulikia ekumeni hasa upande wa Waortodoksi, ikiruhusu kutoleana nao sakramenti kadhaa na mengineyo.

UNITATIS REDINTEGRATIO

Kurudisha umoja kati ya Wakristo wote ni lengo kuu mojawapo la mtaguso. Matengano yaliyokata vipandevipande mwili wa Kristo ni kinyume cha matakwa yake na yanakwaza ulimwengu usiweze kuamini. Siku hizi Mungu ametuhurumia na kututia hamu ya umoja hata ukatokea mfumo wa ekumeni. Kwa hati hiyo Kanisa Katoliki linawajibika kushirikiana na madhehebu yoyote ya Kikristo lisije likazuia kazi hiyo ya Roho Mtakatifu.

Sura ya kwanza inaeleza msimamo wa Kikatoliki kuhusu ekumeni. Imani yetu ni kwamba Kanisa ni moja tu, nalo limekabidhiwa kwa waandamizi wa mitume chini ya waandamizi wa Petro. Tunakiri kuwa mafarakano yaliyotokea kati ya Wakristo yalisababishwa na makosa ya pande zote. Waliolelewa Kikristo nje ya Kanisa Katoliki hawawezi kulaumiwa, tena ni Wakristo halisi na ndugu zetu, ingawa ushirika wetu si kamili. Tuwaheshimu pamoja na mema yao mengi ambayo yanatokana na Mungu na kuelekea ujenzi wa Kanisa. Makanisa yao au jumuia zao vinatumiwa na Mungu kama vyombo vya wokovu, ila katika Kanisa Katoliki tu unapatikana ukweli mzima na vifaa vyote vya wokovu. Hata hivyo tunakiri kwamba hatutumii vizuri neema hizo hata tunawakwaza wenzetu; basi, tunapaswa kulenga ukamilifu wa Kikristo ili Kanisa ling'ae mbele ya wote. Mbali ya matendo ya kupendana ni muhimu pia majadiliano ya kiteolojia na mikutano ya sala ya pamoja.

Sura ya pili inaeleza utekelezaji ikisisitiza kuwa unawapasa waamini wote, kwa njia ya kurekebisha Kanisa, kuongoka, kusali, kushirikishana sakramenti, kufahamiana, kueleza imani kwa usahihi na bila ya kudharau madhehebu mengine, kushirikiana katika kutetea haki na amani na kuleta maendeleo.

Sura ya tatu inaeleza kifupi historia ya mafarakano kwa kutofautiana sana yale yanayohusu Waortodoksi na yanayohusu Waprotestanti, hasa kutokana na makundi hayo mawili kuwa au kutokuwa na daraja halisi na hivyo kuwa au kutokuwa na ekaristi. Kwa msingi huo yanastahili kuitwa Makanisa au jumuia za Kikanisa tu. Uhusiano wetu na makundi hayo ni tofauti, na uwezekano wa kushirikiana katika sakramenti ni mkubwa kwa Waortodoksi bali ni mdogo kwa Waprotestanti.

Mwishoni hati hii inakiri kuwa ekumeni inapita uwezo wetu, kwa hiyo tegemeo lote ni katika sala ya Yesu kwa Kanisa, katika upendo wa Baba na katika uwezo wa Roho Mtakatifu.

CHRISTUS DOMINUS

Mtaguso, baada ya kufundisha wazi juu ya daraja ya maaskofu, ulitunga hati nyingine kuhusu utendaji wao katika ngazi tatu: Kanisa zima, Makanisa maalumu na ujirani mwema wa majimbo.

Kwanza askofu yeyote ni kiungo cha kundi la maaskofu ambalo linaongozwa na askofu wa Roma na kuwajibika kulichunga Kanisa zima. Wajibu huo unatimizwa kwa kushiriki mtaguso mkuu, ambako ni haki ya maaskofu wote, kuchangia muundo mpya wa sinodi ya maaskofu, kushughulikia kwa hali na mali misheni na majimbo yasiyo na mapadri au mali za kutosha, kuwaombea maaskofu wafungwa na wanaodhulumiwa, kuchangia katika ofisi za Papa.

Pili, ni wajibu wa baadhi ya maaskofu kuchunga kwa jina la Bwana sehemu fulani ya taifa la Mungu wakitimiza kazi za kufundisha, kutakasa na kuongoza kama wachungaji halisi, ingawa wanapaswa kuheshimu mamlaka ya Papa, patriarki na maaskofu wakuu. Chini ya askofu wake jimbo ni Kanisa maalumu ambamo Kanisa pekee linaishi na kutenda. Hati hiyo inaelekeza namna ya kutimiza wajibu huo (pamoja na kuagiza utungwe mwongozo maalumu ambao ufafanue zaidi), inaagiza mipaka ya majimbo irekebishwe yasiwe makubwa mno wala madogo mno, na inaratibu uhusiano na maaskofu waandamizi na wasaidizi, nafasi ya makamu na halmashauri za askofu, uhusiano na maparoko na mapadri wengine. Swala lingine gumu ni uhusiano na watawa hasa walio mapadri, ambao wamehimizwa sana kuishi kweli kama viungo vya jimbo na kujihusisha na maendeleo yake ya Kiroho na ya kitume kwa kushirikiana na askofu, mapadri na walei pamoja na watawa wengine. Pia maaskofu wazee au wenye shida nyingine wanahimizwa kujiuzulu.

Tatu, maaskofu wanahimizwa kuchangia ustawi wa Kanisa katika maeneo yao kupitia sinodi, mitaguso ya kanda au ya nchi, mabaraza ya maaskofu, ushirikiano katika kanda, pia na maaskofu waliopewa kazi tofauti na jimbo (k.mf. uchungaji wa askari wote wa nchi yao).

Maagizo yote ya hati hiyo yalikusudiwa kuongoza marekebisho ya sheria za Kanisa.

PERFECTAE CARITATIS

Siku hiyohiyo iliyotolewa hati kuhusu uchungaji wa maaskofu ilitolewa nyingine kuhusu kurekebisha upya maisha ya kitawa, nayo pia msingi wake ni hati Lumen Gentium juu ya Kanisa ambamo watawa wana nafasi yao (sura ya sita). Mtaguso ulitaja marekebisho makuu tu ya kufanywa, ukimuachia Papa atunge sheria hapo baadaye. Hasa ulisisitiza hali mpya ya utawa inayotakiwa kutokana na mambo matano: kushika Injili kama kanuni kuu, kufuata kiaminifu karama ya mwanzilishi na mapokeo bora ya shirika, kujihusisha na maisha na malengo yote ya Kanisa, kupima hali na mazingira ya watu wa leo, kuweka mbele maisha ya Kiroho kuliko mipango mingine. Ili kuzingatia hayo yote, sheria za watawa zirekebishwe kwa kuwahusisha wanashirika wote.

Kabla ya kueleza juu ya aina mbalimbali za utawa, hati hiyo inasisitiza mambo kadhaa yaliyo sawa kwa zote: kushika mashauri ya Kiinjili, kujikatalia ulimwengu, kuwekwa wakfu kwa Mungu juu ya msingi wa ubatizo, kulitumikia Kanisa, kutekeleza maadili, kumfuata Kristo kwa bidii kama jambo pekee la lazima, kuunganisha sala hasa na moyo wa kitume. Nafasi ya kwanza inayo maisha ya Kiroho yaliyo chemchemi ya upendo unaohuisha hata utekelezaji wa mashauri ya Kiinjili. Watawa katika kulisha maisha ya sala wazingatie kila siku Maandiko matakatifu halafu liturujia.

Katika kutofautisha aina za utawa, kwanza yanatajwa mashirika yanayoshughulikia sala tu katika upweke na kimya; baadaye yanatajwa mashirika yale mengi yaliyoanzishwa waitimize huduma maalumu kwa niaba ya Kanisa na kama sehemu ya maisha yao ya kitawa; mwishoni yanatajwa mashirika yanayotakiwa kuunganisha kiaminifu ratiba ya sala na taratibu nyingine za kijumuia pamoja na utume fulani.

Halafu hati inaongelea maisha ya kitawa ya mabradha na masista, ikisisitiza kuwa ni muhimu yalivyo, bila ya kuhitaji yakamilishwe na daraja takatifu. Vilevile inasisitiza sura ya mashirika ya kilimwengu yanayopaswa kutafuta utakatifu kwa kuishi katika mazingira ya watu wa kawaida: kwa ajili hiyo yanahitajika malezi bora.

Baadaye hati inarudi kufafanua mambo yanayowahusu watawa wowote, hasa mashauri makuu matatu ya Kiinjili, ikitanguliza useja kwa kuwa ndio msingi hasa wa kubainisha waliowekwa wakfu kwa Mungu na kwa ufalme wake kwa namna ya pekee. Hati inaonyesha ubora wa useja na njia za kuushika sawasawa baada ya jaribio la kutosha. Halafu inasisitiza ufukara kama ushahidi unaothaminiwa sana siku hizi: basi, usiwe wa kiroho tu au wa binafsi tu, bali uonekane wazi katika maisha ya jumuia pia. Kuhusu utiifu umesisitizwa ukuu wa sadaka hiyo ambayo mtawa anaungana kwa hakika na matakwa ya Mungu kwa mfano wa Yesu. Pamoja na hayo ajitahidi kutoa mchango wake na kuwajibika chini ya viongozi kama mtu aliyekomaa. Upande wao viongozi wasitawale kwa mabavu bali waonyeshe upendo

wa Mungu kwa mtawa, wakimheshimu na kumsikiliza na kumuachia nafasi ingawa wana haki na wajibu wa kumuagiza la kufanya. Pia mikutano na halmashauri vishiriki katika uongozi.

Sifa nyingine ya mashirika ya kitawa ni maisha ya pamoja ambayo yamesisitizwa upya kwa kutia maanani misingi yake na utekelezaji wa upendo kamili katika ushirika wa kidugu. Kwa lengo hilo tunakuta himizo la kufuta matabaka kati ya masista na la kushirikisha zaidi mabradha katika maisha ya jumuia, pamoja na kibali cha kuleta usawa kati ya wanashirika makleri na walei.

Katika kulinda utawa toka zamani unatumika ugo, ambao kwa baadhi ya watawa wa kike unafuata sheria za Papa. Hati hii inadai hizo zirekebishwe, halafu zisibane wale wanaofanya utume fulani. Kinga nyingine ya watawa ni nguo maalumu. Kwa mara ya kwanza katika historia mtaguso uliongelea swala hilo na kulitia maanani kama alama ya kuwekwa wakfu, pamoja na kuagiza baadhi zibadilishwe.

Upande wa malezi hati hii imeyasisitiza sana kama msingi wa urekebisho, ikikataza watawa wasitumwe kufanya shughuli mara baada ya unovisi, bali waendelee kuundwa katika nyumba maalumu. Halafu malezi yaendelee maisha yote kwa ushirikiano wa watawa na viongozi wao, ambao wajitahidi hasa kuandaa walezi wa kufaa.

Zinafuata taratibu kuhusu kuunda mashirika mapya, halafu kuhusu kueneza aina mbalimbali za utawa katika Makanisa machanga kwa kuzingatia utambuzi na utamadunisho. Mashirika yaendelee kutimiza shughuli zake maalumu kulingana na karama na nyakati pamoja na kustawisha moyo wa kimisionari. Yale yasiyostawi yakatazwe yasipokee tena wanovisi au yaunganishwe na lingine la kufanana nayo. Tofauti na muungano, mtaguso umependekeza pia shirikisho la monasteri au mashirika ya familia moja ya kiroho, vyama vya mashirika yenye kazi ileile, mabaraza ya wakuu wa mashirika yote ya nchi au jimbo fulani ili kurahisisha ushirikiano kati ya watawa, tena kati yao na maaskofu.

Swala la mwisho ni namna ya kupata miito ya kitawa: hiyo ni kazi ya Kanisa lote, kuanzia mapadri, wazazi na walezi. Mashirika yenyewe yanaweza kujitafutia miito kwa kufuata taratibu za Kanisa, lakini njia bora ni kutoa mfano mzuri. Hatimaye watawa wote wanahimizwa kuitikia upya wito wao.

OPTATAM TOTIUS

Siku hiyohiyo ilitolewa hati nyingine tena inayohusu malezi ya kipadri: toka mwanzo hayo yanatiwa maanani sana kwa kusema urekebisho unaotumainiwa wa Kanisa lote unategemea kwa kiasi kikubwa upadri ukitimizwa kwa roho ya Kristo. Kuhusu jambo hilo mtaguso ulikusudia kulinganisha mang'amuzi ya karne zilizopita na mahitaji mapya. Kwa kuwa malezi yanapaswa kuwa tofauti kwa kila mtu na kila aina ya watu, basi maagizo ya hati hiyo yanayolenga kulinda umoja wa upadri, yatekelezwe kwa namna tofauti kadiri ya mazingira, madhehebu na aina ya upadri (watawa, wanajimbo waseja na wenye ndoa).

Kwanza jumuia nzima inapaswa kuwajibika kwa malezi ya vijana na ustawi wa miito hasa kwa njia ya sala. Wakurugenzi wa miito wasishindanie vijana, bali tujifunze wote kuwa na mtazamo wa Kikanisa na wa kimataifa. Njia ya kawaida ya kuotesha mbegu za miito ni seminari ndogo. Hizo si za lazima, kinyume na seminari kuu ambapo malezi yote yanalenga upadri moja kwa moja. Walezi wachaguliwe kati ya mapadri bora, kwa kuwa malezi yanawategemea hasa wao. Waseminari waendelee kuchambuliwa kwa imani ya kwamba Mungu hatakubali Kanisa likose wahudumu ikiwa wasiofaa wanaelekezwa kwingine. Namba nyingine zinahusu malezi ya kiroho, upendo kwa Kanisa, malezi ya kijinsia, ukomavu wa kibinadamu na uwezekano wa marekebisho ya sheria. Yanafuata maagizo kuhusu masomo yenyewe ambayo moyo wake uwe ni Biblia, na masomo ya juu. Pia inasisitizwa kuwa masomo na malezi hayo yote yanalenga uchungaji katika nyanja zote.

APOSTOLICAM ACTUOSITATEM

Mtaguso uliwaongelea walei katika hati mbalimbali ukionyesha nafasi yao katika maisha ya Kanisa (liturujia, upashanaji habari, ekumeni n.k.). hata hivyo uliona umuhimu wa kuwaandikia hati maalumu iwaongoze hasa katika utume ili watimize wajibu wao kwa wokovu wa ulimwengu. Karibu waamini wote ni walei, tena ndio wanaoshirikiana zaidi na watu wowote katika yote: hivyo wasipotoa mchango wao, utume wa Kanisa utakuwa mlemavu, hasa siku hizi. Si kwamba wanapaswa kufanya utume kutokana na upungufu wa mapadri na watawa, bali kutokana na wito walioupata katika ubatizo na kipaimara.

Sura ya kwanza inaeleza wito huo katika Kanisa na roho itakayowawezesha kuutimiza kitakatifu, kwa sababu wito wao ni tofauti na ule wa mapadri na watawa, hivyo maisha ya Kiroho pia yanapaswa kuwa tofauti.

Sura ya pili inaeleza malengo makuu ya utume wa walei, kwamba sio tu kueneza ujumbe wa Kristo, bali pia kuratibu malimwengu yafuate matakwa ya Mungu, kutimiza matendo ya huruma na kushuhudia upendo.

Sura ya tatu inafafanua zaidi nafasi mbalimbali za utume wao: jumuia za Kikanisa, familia, vijana, jamii, taratibu za kitaifa na za kimataifa.

Sura ya nne inaeleza namna za kutimiza utume, kuanzia ule wa mtu mmojammoja hadi ule wa pamoja katika vyama mbalimbali ambavyo walei wana haki ya kujiundia, na katika miundo maalumu iliyoanzishwa na wachungaji wao.

Sura ya tano inaeleza utaratibu wa kufuatwa katika utume ili ufanyike si kwa wivu na mashindano bali kwa upendo na ushirikiano, kwanza na maaskofu, mapadri na wahudumu wengine mpaka na Wakristo wa madhehebu tofauti na wasio Wakristo. Kwa ajili hiyo katika ngazi zote iwepo halmashauri.

Hatimaye *sura ya sita* inasisitiza haja ya malezi bora kuanzia utoto na ujana na katika nyanja zote zinazohusu utu na Ukristo. Halafu yawepo malezi maalumu kwa ajili ya shughuli maalumu.

AD GENTES

Siku ya mwisho kabla ya kufunga mtaguso zilitolewa bado hati tatu, mojawapo kuhusu umisionari wa Kanisa, aina ile ya utume inayowaelekea watu wengi zaidi (thuluthi mbili za watu wote) yaani wasio Wakristo. Kazi hiyo ni tofauti na uchungaji (unaowaelekea Wakatoliki) na ekumeni (inayowalenga Wakristo wengine).

Sura ya kwanza inafafanua misingi ya umisionari: kwanza upendo wa Baba uliomfanya amtume Mwana halafu kwa jina lake amtume Roho Mtakatifu kwa Kanisa lililotumwa na Yesu kuendeleza kazi yake. Basi, umisionari unatokana moja kwa moja na maumbile ya Kanisa, pamoja na kudaiwa na azimio la Mungu la kutaka watu wote waokoke na kujua ukweli. Kwa umisionari tunawakusanya pia watu katika umoja na kuharakisha ujio wa ufalme wa Mungu.

Sura ya pili inaeleza utendaji wenyewe kwanzia ushuhuda wa maisha ya Kikristo na wa matendo yaliyojaa upendo. Kwa ajili hiyo waamini wahusiane na kujadiliana vema na watu wengine. Juu ya msingi huo inaweza kufanyika kazi ya kuwahubiria Injili na kuwakusanya katika taifa la Mungu. Hati hii inakataza katakata tusiwalazimishe wala kuwavuta kwa udanganyifu wakubali imani, kama tunavyodai wasizuiwe kufuata imani. Baada ya kuchunguza na kunyosha sababu za uongofu wao, waliojaliwa mwanzo wa imani wapokewe kwa ibada maalumu katika ukatekumeni ambao ufuate maagizo mbalimbali ya mtaguso. Waliobatizwa wanatakiwa kuishi kijumuia kama familia ya Mungu, ambayo itie mizizi kweli katika makabila ya mahali, hasa kwa njia ya walei. Pamoja nao Kanisa, likilenga mara kujitegemea iwezekanavyo katika miundo yote, linahitaji zaidi na zaidi wahudumu wanaotokana na makabila hayo mpaka liundwe jimbo lenye askofu, mapadri, mashemasi, watawa na makatekista wenyeji.

Sura ya tatu inajadili Makanisa maalumu ikionyesha jinsi yale machanga yanavyoendelea na kukomaa hata kuanza kuwatuma mapadri, watawa na walei walio tayari kwenda kwa wasio Wakristo, ndani ya jimbo na nje pia. Hivyo Kanisa lililokomaa katika mazingira yake linashirikisha utajiri wa nchi yake, badala ya kuishia kukidhi mahitaji yake tu.

Sura ya nne inazungumzia wamisionari wenyewe, malezi yao na maisha ya kiroho yanayopaswa kulingana na wito wao maalumu. Ili kurahisisha malezi hayo na kazi hiyo Mungu alitokeza pia mashirika yenye umisionari kama lengo kuu.

Sura ya tano inatoa maagizo ili umisionari uwe na umoja na kufanikiwa. Kimataifa Papa aratibu umisionari kwa njia ya idara ya uenezaji imani, isipokuwa Makanisa ya mashariki yanafuata idara yao. Vilevile kijimbo na kitaifa kuwe na miundo na ushirikiano kati ya mashirika.

Sura ya sita inapanua mtazamo kwa kuonyesha kuwa umisionari unahusu Kanisa lote kama wajibu wake mkuu. Kwa hiyo ni lazima kila mwamini ajirekebishe na kuchangia wokovu wa wasio Wakristo. Vilevile kila jumuia iwashughulikie walio mbali kwa bidii ileile inayowashughulikia walio jirani. Kwa namna ya pekee wanapaswa kuwajibika maaskofu kama waandamizi wa mitume waliowekwa wakfu kwa wokovu wa ulimwengu mzima. Baada yao mapadri waeneze moyo wa kimisionari ili miito ya namna hiyo ipatikane na michango ifanikiwe. Tena mashirika yote ya kitawa, yawe ya sala tu au ya utume, yafikirie upya yanavyowajibika katika umisionari. Mwishoni walei pia wana nafasi kubwa katika kazi hiyo nchini kwao na kwenye misheni za mbali.

PRESBYTERORUM ORDINIS

Hati hiyo pia ilitolewa siku ya mwisho kabla ya kufunga mtaguso ili kufafanua tena mambo kadhaa yaliyokwishaelezwa katika hati nyingine.

Sura ya kwanza inahusu upadri katika utume wa Kanisa, jinsi unavyounganisha mapadri na maaskofu kwa ajili ya taifa la Mungu.

Sura ya pili inaeleza kwanza zile kazi tatu za mapadri, yaani kufundisha, kutakasa na kuongoza. Halafu inasisitiza uhusiano wao na askofu, kati yao, tena na walei. Mwishowe inafikiria la kufanya ili kuwe na mapadri wa kutosha: hiyo haitegemei tu bidii kwa ajili ya miito, bali pia ugawaji mzuri wa watenda kazi katika shamba la Bwana.

Sura ya tatu inaingia zaidi katika maisha yao ikisisitiza wanavyopaswa kwa namna ya pekee kulenga utakatifu, na kuutafuta hasa kwa kutekeleza vema huduma zao na kuziunganisha katika

kutimiza matakwa ya Baba kama Yesu alivyofanya. Kati ya maadili wanayoyahitaji, hati inaeleza hasa mashauri ya Kiinjili ya utiifu, useja na ufukara ambayo kwao yanalenga ubora wa huduma za kipadri (tofauti na watawa wanaoyashika kwanza ili kujipatia utakatifu). Kwa sababu hiyo la kwanza kwa mapadri ni utiifu, kumbe useja si wa lazima (tunavyoona katika Kanisa la mwanzoni na katika Makanisa ya mashariki mpaka leo). Baada ya hapo hati inakabili swala la kuwasaidia kwa namna mbalimbali: kwanza katika maisha ya Kiroho, halafu kuhusu elimu hasa ya kidini, lakini pia kuhusu malipo ya haki na bima wasije wakahangaika. Mwishoni mapadri wanatiwa moyo katika magumu yanayowakabili siku hizi, kwa kukumbusha kinachojulikana kwa imani tu, kwamba Mungu na Kanisa wapo pamoja nao.

GRAVISSIMUM EDUCATIONIS

Katika tamko hilo la kwanza mtaguso ulizingatia umuhimu wa malezi kwa mtu binafsi, kwa jumuia zake, kwa nchi yake na kwa Kanisa lenyewe. Watu wa leo wanaelewa zaidi umuhimu huo kwa watoto, vijana na hata watu wazima; ndiyo maana wanafanya mipango mingi wakitumia pia njia mpya zilizoletwa na maendeleo. Kanisa linataka kuchangia juhudi hizo kufuatana na wajibu wake kwa watu wote na kwa mtu mzima (mwili na roho).

Hati hiyo inasisitiza haki ya kila mtu kupata malezi ya kumfaa; halafu waamini wote wana haki ya kupata malezi ya Kikristo, hasa vijana, tumaini la Kanisa. Wazazi ndio walezi wakuu kwa watoto wao: wasipoutimiza wajibu huo mkubwa, si rahisi kujaza pengo hilo. Familia isaidiwe na jamii na Kanisa kwa njia mbalimbali, hasa shule: walimu waone kazi yao kuwa ni wito. Ni juu ya wazazi kuchagua kwa hiari aina ya shule inayohakikisha watoto wao walelewe wanavyopenda wazazi wenyewe. Serikali haina haki ya kulazimisha wote kupata malezi ya aina moja, bali inapaswa kusaidia shule huru za wazazi na za kidini.

Kanisa liwashughulikie Wakristo wanaosomea shule zozote, lakini lijitahidi kuwaanzishia shule za kwake likiwahimiza wazazi kuwaandikisha watoto wao katika shule hizo. Katika shule katoliki elimu ya kawaida itolewe katika mazingira ya imani ili kijana alelewe bila ya mgawanyiko wa ndani. Shule katoliki zinaweza kupokea pia wanafunzi wasio wa dini yetu na kuwa za namna mbalimbali na za ngazi zote, kuanzia za chekechea hadi vyuo vikuu, pamoja na vyuo vya kufundishia dini tu. Kati ya shule hizo zote ushirikiano ni muhimu.

NOSTRA AETATE

Kutokana na mchanganyiko wa watu ambao siku hizi unaongezeka mahali pengi, mtaguso uliona haja ya kutoa tamko juu ya uhusiano na dini mbalimbali ili kujenga umoja kadiri ya mpango wa Mungu.

Tamko hilo linasema kwanza juu ya dini za kimila, halafu juu ya dini zilizoendelea pamoja na elimu (k.mf. Ubaniani na Ubudha): Kanisa linaheshimu dini hizo, ambazo ni tofauti sana na ya kwetu, ila linazidi kuwatangazia wote kuwa Yesu ndiye njia, ukweli na uzima.

Katika nafasi ya pekee unasifiwa Uislamu kwa tunu zake nyingi. Mtaguso ukizingatia magomvi ya zamani kati ya Wakristo na Waislamu umewahimiza wote kusahau yaliyopita na kuanza kuelewana na kushirikiana.

Mwishoni tamko linasifu Israeli likihimiza wote kufahamiana vizuri na Wayahudi na kuacha kuwalaumu kwa makosa wasiyonayo. Kanisa linalaani dhuluma yoyote dhidi yao ambao toka zamani wameteswa mno hata na Wakristo na kwa visingizio vya Kiinjili. Kumbe bado ni wapenzi wa Mungu, nasi tunalishwa na utomvu wa mizizi yao.

Basi ni juu yetu kuondoa ubaguzi wowote na kujenga udugu ili tuwe kweli wana wa Mungu.

DIGNITATIS HUMANAE

Tamko hilo la mwisho lilisababisha mijadala mikali wakati wa mtaguso na baada yake hata likachangia kwa kiasi kikubwa farakano la askofu Lefebvre. Sababu ni kwamba linasisitiza haki ya binadamu ya kufuata ukweli wa kidini kadiri alivyoujua, wakati mafundisho ya zamani yalikuwa yakisisitiza kuwa imani ya Kikristo ni ya lazima kwa wokovu. Lakini masisitizo hayo hayapingani, kwa maana ni wajibu wa kila mtu kuutafuta ukweli na kuufuata, ila hatuwezi kumlazimisha asiyejaliwa bado imani au mwanga wa kutosha, bali tunapaswa kuendelea kumtangaza Yesu kwa wokovu wa watu.

Kinyume cha baadhi ya matendo ya Wakristo wa zamani, Kanisa linaamini kwamba dini yetu inapaswa kuenea kwa nguvu ya ukweli wake, sio kwa upanga, kwa kuwa Mungu mwenyewe anamheshimu binadamu na hiari yake. Mfano bora ni ule wa Kristo na wa mitume wake.

Basi, kila mtu na kila serikali waheshimu uhuru wa kufuata dini yoyote. Haki hiyo inahusu mtu binafsi na makundi pia.

MTAKATIFU FRANSISKO NA MTAGUSO

Mzee wetu Fransisko anasifika kwa ukatoliki wake: alishikamana kabisa na Kanisa akiwatii viongozi wake na kuwa rafiki yao. Tangu mwanzo alitaka kuweka utawa wake chini ya Mama Kanisa Takatifu la Roma akakubaliwa kwa moyo. Kinyume cha uzushi mwingi wa wakati wake, karama ya Fransisko ilionyesha wazi kuwa Injili imekabidhiwa kwa Kanisa, hivyo ishikwe kikamilifu ndani ya Kanisa na kwa msaada wake.

Tukiangalia zaidi uhusiano huo tunaona kuwa Fransisko aliingia kabisa katika juhudi za urekebisho wa liturujia na maadili ambazo kilele chake ni mtaguso wa nne wa Laterano (1215). Wengi wanadhani kuwa mwenyewe aliuhudhuria akiwa ni mkuu wa utawa; kwa vyovyote ni hakika kuwa baadaye alionekana kujua sana malengo na maamuzi ya mtaguso huo, na kutaka kuyatekeleza pamoja na wafuasi wake na waamini wote.

Kwa mfano, barua zake zinahimiza heshima kwa ekaristi na kwa yale yote yanayohusu liturujia: katika kuziandika alitumia hata maneno yenyewe ya hati za mtaguso na za Papa. Zaidi tena, Fransisko alipokea kwa moyo mpango wa Inosenti III wa kufanya Kanisa lote (hasa makleri) liongoke kwa kusulubisha mwili na tamaa zake, likitumia ile tau inayoongelewa na Ezekieli 9 kuwa ni muhuri waliotiwa wateule wa Mungu waliokubali msalaba katika maisha yao. Hivyo tau ikawa kwa Fransisko pia ishara ya toba aliyojitahidi kuieneza kati ya waamini. Kwa kuungana kabisa na Msulubiwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu katika yote, akawa chombo cha kurekebishia Kanisa si kwa kulilaumu wala kwa kulipinga, bali kwa njia ya utakatifu.

Kwa namna fulani Kanisa linajikuta leo katika nafasi inayofanana na ile ya zamani za Fransisko na linahitaji watu ambao wamefanywa wapya kwa kushiriki mateso ya Kristo, na ambao Roho aweze kuwatumia bila ya pingamizi kwa ujenzi wa ufalme wa Mungu. Mtaguso wa pili wa Vatikano umepanga kwa upana wote kazi ya kutengeneza upya maisha ya Kikristo, lakini kazi hiyo haiwezi kufanyika bila ya mwanga na nguvu ya Roho Mtakatifu, naye anafanya kazi hasa katika watu waliokubali kujazwa naye hata kuwashirikisha ndugu zao.

Basi, mfano wa Fransisko unawahimiza Wakristo washikamane na Kanisa kwa nguvu zao zote; ndani yake mfumo au muundo wowote usikubali kuwa na mpango wake wenyewe, bali utumie kwa unyenyekevu karama yake katika kutimiza mpango uliofanyika katika mtaguso kwa ushirikiano wa Roho na maaskofu wote. La sivyo miongozo na maagizo yake bora yatabaki maandishi matupu ambayo hayazai matunda yale yote yaliyotarajiwa. Hasa Kanisa linatazamia kuwa wafuasi wote wa Fransisko watatoa mchango wa utakatifu wao ambao kwa namna fulani umfufue kwa ulimwengu wa leo.